www.cdlidd Januari-Machi 2017

# Unabii Wa Habari Za Biblia

## Je,Rais Donald Trump Yuawezakuwa Maangamizi ya Kinabii?



Jinsi ya Kushinda Uwoga Wako

Rekodi Katika Jiwe

# Unabii wa Habari za Biblia *Katika toleo hili:*

**2. Kutoka kwa Mhariri:Je,Rais Donald Trump Yuawezakuwa Maangamizi ya Kinabii**? Mwombee Donald Trump.

**12. Jisomee Kozi ya Biblia Somo la 11.Rekodi katika Jiwe**.Je,uumbaji unathibitisha kwamba Biblia ni ukweli?

**30. Vidokezi Ishirini na Nane vya Maombi Yanayofaa:Sehemu ya 6**.Je,ungependa kujifundisha jinsi ya kufanya maombi yako yafae zaidi?

Jalada la Nyuma:Intaneti na Redio:Hii inaonyesha watu mahali pa kupata ujumbe wa Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG).

Kuhusu Jalada la Nyuma.Hii ni picha na Michael Vadon ya Donald Trump aliyechaguliwa kuwa Rais wa 45 wa Mataifa ya Muungano wa Marekani.

Unabii wa Habari za Biblia inachapishwa na Kanisa la Mungu Linaloendelea(CCOG),1036 W.Grand Avenue,Grover Beach,CA,93433.https://www.ccog.org

(c) 2017 Kanisa la Mungu Linaloendelea.Imechapishwa U.S.A.Haki zote zimehifadhiwa.

Kunakili makala yote ama sehemu yake pasipo ruhusa ya kimaandishi toka kwa mmiliki hairuhusiwi.Tunaheshimu haki zako hivyo hatutoi,kuuza ama kukodisha orodha ya mawasiliano yetu.Endapo haungependa kuendelea kuupokea gazeti hili,wasiliana na afisi yetu ya Grover Beach.Maandiko yamenukuriwa toka New King James version (c) Thomas Nelson,Inc,Publishers,used by permission isipokuwa pale tu tumeelekezwa vinginevyo.

**Unabii wa Habari za Biblia HUWEZESHWA KWA MICHANGO YENU.**

**Mhariri Mkuu:Bob Thiel**

**Makala/Mhariri Msaidizi:Joyce Thiel**

**Mashahihisho:John Hickey;SBC Course Assister;Shirley Gestro.**

**Picha:Picha zote zimetokana na familia ya Thiel ama na vyanzo vya mitandao ya kijamii kama vile Wikipedia (ikiwa ni chanzo haikutajwa;itakuwa ni kwa sababu inaaminika kwamba chanzo husika kiliachia picha iwe matumizi ya umma pasipo masharti yoyote)**



**KUTOKA KWA MHARIRI MKUU: BOB THIEL**

## Je,Rais Donald Trump Yuawezakuwa Maangamizi ya Kinabii? Mwombee Donald Trump!

Uchaguzi wa mwanzo na uchaguzi kwa jumla wa urais katika mwaka wa 2016 Marekani ulikuwa wa ajabu mno na pengine wa kutenganisha sana ambao nimeuona.

Haya yaliyonenwa,licha ya kashfa,uchunguzi,na maelezo yasiyofaa,Donald Trump alichaguliwa kama Rais wa awamu ya 45 wa Marekani.Bila shaka,mgombea mwenza alikuwa na kashfa mbalimbali,uchunguzi na maelezo yasiyofaa pia.

Biblia inaonya:

> 17 Hukumu hii imekuja kwa agizo la walinzi,na amri hii kwa neno la watakatifu;kususdi walio hai wapate kujua ya kuwa Aliye juu anatawala katika ufalme wa wanadamu,naye humpa amtakaye,tena humtawaza juu yake aliye mnyonge.(Danieli 4:17 NLT)

Katika kipindi hiki cha uchaguzi,ilikuwa wazi kwangu kwamba Mungu ataamua atakaye kuwa Rais .

Haijalishi unachohisi kuhusu urais wa Donald Trump,ukiwa Marekani unatakikana umwombee Rais.Na hata kama wewe siye wa Marekani inabidi pia uwaombee viongozi wa kisiasa:

> 1 Basi,kabla ya mambo yote,nataka dua,na sala na maombezi,na shukrani,zifanyike kwa watu wote;2 kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka,tuishi maisha ya utulivu na amani,katika utauwa wote na ustahivu.3 Hili ni zuri nalo lakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu (I Timotheo 2:1-3).

Kama vile nilivyoandika katika toleo la awali ya makala hii,haijalishi aliyechaguliwa,kwa ajili ya wakati huu,wote wangekuwa maangamizi ya kinabii (wangefanya vitu ambavyo vinaongoza kwa utimizaji wa unabii) na kutimiza unabii mbalimbali wa nyakati za mwisho ( 2 Timotheo 3:1-5).

Kwa Donald Trump hili  linabaki kuwa la ukweli:

Haswa,hizi ni sababu 13 zinazofanya Donald Trump kuzingatiwa kuwa ‘’Maangamizi ya kinabii’’.

1.Wakati wa kuchipuka kwake katika umaarufu wa kisiasa.Miaka 6,000 Mungu aliwapa wanadamu kuamua mambo yake inakaribia kuisha.Tuko katika siku za mwisho ya mpango wa Mungu.Siku kwa Mungu ni kama  miaka 1,000 (2 Petro 3:8; Zaburi 90:4),na kwa sababu ni bora kujua siku (Zaburi 90:12),hii ni sababu inayofanya Donald Trump kuwa maangamizi ya kinabii.Kuna uwezekano kwamba imebaki awamu tatu ya urais kabla ya kuanza kwa Dhiki Kuu na utimizaji wa unabii katika kitabu cha Ufunuo.Kwa ajili ya majira yake ( na pia mpango wake halisi na matendo yake yasio na mpango)  inatosha kusababisha utimizaji wa unabii tofauti ya nyakati za mwisho.

2.Donald Trump tayari amekasirisha Wazungu wa Ulaya,na biashara yake na sera zingine,hata hivyo wengine wanakubaliana naye.Taarifa zake zingine zinaweza kusababisha kuinuka kwa mfalme wa Kaskazini kama vile ilivyotabiriwa,ambaye ni kiongozi wa mwisho wa Mnyama wa Ufunuo

(Ufunuo 13:1).Wengine katika Uropa wamengojea kwa hamu kuinuka kwa Donald Trump kwa ajenda yao wakiamini **''Trump anawakilisha fursa moja muhimu katika kizazi cha ukombozi kutoka kwa ushawishi wa Marekani''** (Kwa nini Uropa wanaweka shina la Donald Trump.ZH,9/23/16) na wengine wanasema kuwa uchaguzi wake unaonyesha ''Zamu ya Uropa'' ya kuongoza eneo la Magharibi (Marekani wameng'atua uongozi wao wa Magharibi.*Der Spiegel* 11/14/16).Biblia inafundisha kwamba Uropa litakuwa na ''jeshi kubwa'' (Daniel 11:25) na baadaye litaharibu ''ngome zenye nguvu'' (Danieli 11:39),ambayo ni Marekani).

3.Katika 2015,Donald Trump haswa alisema kwamba hajatubu.Mungu wa Biblia anatarajia viongozi kuhimiza toba na maadili mema wakati wako chini ya adhabu kali (Yona 3:6-9).Donald Trump,kama vile wanasiasa wengine wengi wa Marekani,haonekani kuamini kwamba Marekani wanahitaji toba kwa dhambi zao dhidi ya Mungu.Hata hivyo,bila toba ya kimataifa,Marekani watapata adhabu ya uharibifu (Isaya 30:12-13;Danieli 11:39).

4.Kwa kulenga sana tishio kutoka China na pia kila mara akidhania wazungu wa Ulaya kuwa wasaidizi,utawala wa Donald Trump wakati huu hautaraji kugeuza mkakati wa ''egemeo'' la Asia.Asipobadili hili,egemeo hili litasaidia katika uharibifu wa Marekani.

5.Donald Trump ametoa taarifa zinazopendekeza kuwa anapendelea serikali isiyo na mpaka wa kufuatilia.Aina ya kitu kama hiki kitanyonywa na 666 ya Ufunuo 13:16-18.

6.Tuko katika kipindi cha ukaguzi wa kibinafsi na ukaguzi wa kiserikali. ''Njaa'' ya neno ilitabiriwa (Amosi 8:11) na utawala wa Donald Trump unaweza kuamuru taarifa,kupiga chapa,Intaneti,na/ama kizuio ukijaribu kuwa na mamlaka ya kuamuru zaidi.

7.Donald Trump anachukuliwa kuwa msinzi,anayemiliki shirika la kuvua nguo na kasino na alioa mwanamke anayeshughulika katika ponografia(biashara ya ngono).Kwa kuhimiza badala ya kukemea suala la uasherati kibiblia,Donald Trump anaweka Marekani katika adhabu ( Isaya 30:12-13;Warumi 1:18-32) ambayo italeta taabu,vurugu,shida za hali ya hewa,tetemeko la ardhi,ukosefu wa chakula na maradhi (Mariko 13:7-8;Luka 21:10-11).Siku zinakuja ambapo shida hizi zitaongezeka zaidi.

8.Donald Trump mara nyingi amesema kwamba ''atafanya Marekani mkuu tena.''Kibiblia hajatoa sababu zake kwa tamko hilo.Kimaadili,kiuchumi,na kijeshi Marekani imekuwa katika upungufu (hata hivyo upungufu wa kijeshi umekuwa kwa sababu ya wengine wanaopanda).Biblia inaonya mara nyingi kwamba azimio la uwongo la amani litaongoza kwenye uharibifu wa nyakati za mwisho (1 Wathesalonike 5:3;Jeremia 6:14-15).

9.Maoni yake mabaya,kubadili msimamo wake,na mashambulizi dhidi ya wanaomchokoza,inanionyesha kwamba siye mwaminifu.Hili litasababisha watu kuugua (Mithali 29:2).Kauli zake za kujivunia,nk.ni sambamba na zile Biblia inatuonya katika 1 Timotheo 3:1-6.

10.Mtazamo wake wa kidini unadokeza kwamba kiasi ni ''mtu anayeunga harakati ya ekumeni (yaani muungano wa madhehebu)''.Nguvu ya ekumeni imeonywa katika Biblia na inatarajiwa kuinuka juu katika nyakati za mwisho (Zekaria 2:6-9;Ufunuo 17:18).Namtarajia kutoa kauli zaidi ya kutekeleza ekumeni.

11.Donald Trump amekuwa umbo la kingamizi cha mabadiliko na ameudhi wengi pamoja na walio wachache na Waislamu.Tarajia machafuko ya kiraia na ghasia.Biblia inatabiri

**''Kutakuwa na upanga ndani ya vyumba''** (Kumbukumbu 32:25).Biblia haswa inaonya kuhusu shida kutoka Warabu katika nyakati za mwisho (Zaburi 83:3-8).Washuru wengine tayari wako Marekani,wanaweza kufanya matendo ya ugaidi kwa sababu hayo pia ni sambamba na unabii wa kibiblia (Isaya 9:8-9,11-12).

12.Donald Trump ni mlafi,mwenye majivuno na anayejaa kiburi.Biblia inasema, ''nanyi jueni ya kwamba hiyo dhambi yenu itawapata hapana budi'' Hesabu 32:23,na kwamba ''Kiburi hutangulia uangamivu;Na roho yenye kutakabari hutangulia maanguko.'' (Methali 16:18).Kumbuka alichosema Donald Trump katika hotuba yake ya ushindi kule Nevada usiku wa Februari 23,2016:

> *Ni ngumu kwangu kuacha kutafuta pesa kwa sababu hiyo ndiyo nimefanya maishani mwangu mwote,nanyakua,na kunyakua na kunyakua.Mnajua nazidi kuwa mlafi nataka pesa,pesa.*
>
> *Nitawaambia tunachoenda kufanya,sivyo? Tuwe walafi sivyo? Sasa tunaenda kuwa walafi Marekani tunaenda kunyakua na kunyakua na kunyakua.Tunaenda kuleta pesa nyingi na vitu vingi.Tunaenda kufanya Marekani kuwa kuu tena,wenzangu,nawaambia wenzangu tunaenda kufanya Marekani kuwa kuu tena...*
>
> *Mtajivunia Rais wenu,na mtazidi kujivunia nchi yenu,Sawa?*

Kumbuka kwamba Donald Trump anasema waziwazi kuwa ni mlafi anayependa pesa.Mtume Paulo aliongozwa na Roho kuandika:

> '' 1 Lakini ufahamu neno hili,ya kuwa siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari.2 Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe,wenye kupenda fedha,wenye kujisifu,wenye kiburi,wenye kutukana,wasiotii wazazi wao,wasio na shukrani,wasio safi,3 wasiowapenda wa kwao,wasiotaka kufanya suluhu,wasingiziaji,wasiojizuia,wakali, wasiopenda mema,4 wasaliti,wakaidi wenye kujivuna,wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu;5 wenye mfano wa utauwa,lakini wakikana nguvu zake;hao nao ujiepushe nao.'' ( 2 Timotheo 3:1-5)

13.Historia ya Donald Trump ya taflisi inaonyesha kwamba hana haja na kulipa deni.Biblia hufundisha, ''Asiye haki hukopa wala halipi'' (Zaburi 37:21).Marekani ndiyo nchi yenye deni kubwa na Biblia inaonya kuhusu uharibifu wa nchi iliyo na deni kubwa katika wakati unaofaa wa mwisho(Habakuki 2:1-8).Ikiwa Donald Trump ataongeza deni hiyo na/ama kukosa kulipa deni hiyo,hii itafyatua mwisho wa Marekani (Habakuki 2:6-8).

Wakristo pia waombee viongozi wao wa nchi (1 Timotheo 2:1-3). Nimekuwa nikiombea Rais mteule Donald Trump na natarajia wote wanaozingatiwa kuwa Wakristo pia wafanye hivyo.

Je,hili laweza kusaidia Marekani?

Bila shaka.

Kumbuka kwamba Danieli alitiwa msukumo kumwambia Mfalme Nebukadreza:

> 27 Kwa sababu hiyo Ee mfalme,shauri langu lipate kibali kwako;ukaache dhambi zako kwa kutenda haki,ukaache maovu yako kwa kuwahurumia maskini;huenda ukapata kuzidishiwa siku zako za kukaa raha.(Danieli 4:27)

Ikiwa Donald Trump atamgeukia Mungu,na wengi Marekani pia,basi ‘’huenda wakapata kuzidishiwa siku zao za kukaa raha.’’ Tunakaribia mwisho na kwa sababu ya ushawishi mkubwa Marekani wanao ulimwenguni,na pia kilichotabiriwa kitawatukia (k.v. Danieli 11:39),Donald Trump ni maangamizi ya kinabii.Omba.

**Jinsi ya Kushinda Hofu Zako**




Na Dk.Herman Hoeh ( katika 1955 wa Kanisa la Mungu la Redio/Radio Church of God)

Je,unayo shaka kuhusu kushikilia ajira yako? Je,unayo wasiwasi juu ya kupoteza pesa-ama juu ya kukosa pesa unayohitaji? Je, hofu ya maradhi ama kuchanganyikiwa akili ama wazimu inakusumbua?

Je,kuvunjika kwa urafiki,ama kuzimika kwa masuala ya mapenzi yanakunyang’anya afya? BASI UNAYOHITAJI KUFANYA NI HII!

HAKUNA katika historia ya ulimwengu wakati ambapo watu wamefurahia vifaa vingi vya kurahisisha kazi,burudani kwa wingi na kufaidika kutoka kwa usafi wa mazingira ya umma.Na bado,na ni ajabu kusema,hofu ya kuchanganyikiwa akili,magonjwa ya moyo,saratani na wazimu yananyang’anya mamilioni afya njema na furaha.

Watu kila mahali wana matatizo ya kiakili yasiyofaa.Mashinikizo ya biashara na shida za kifamilia zinatia hofu mamilioni.Hatujui jinsi ya kuburudika.Kwa nini kuna mahangaiko,na matatizo ya kiakili? Kwa nini tunashindwa kumudu hofu na wasiwasi?

**Zama za Kutumia Mawazo Vibaya**

Hii si zama za atomu na bomu ya haidrojeni peke yake.Hii ni zama za KUTUMIA MAWAZO VIBAYA!

Mawazo yasiodhibitiwa na yasio na mwelekeo yanaangamiza maisha ya maelfu ya watu wasiohesabika.Mamilioni zaidi wanadunishwa na kukosa faida kwa sababu mawazo yao yametiwa utumwani na HOFU-hofu isiyohitajika,isiyo na sababu!

Hofu isiyohitajika inatunyang’anya hali ya kuridhika,kupinda hulka yetu na kutia sumu mawazo na mwili wetu.

Hofu ni hisia-hisia inayoelekezwa kwa NAFSI.Umewai kugundua kwamba wale wanaoteseka sana kutoka kwa hofu na wasiwasi ‘’wanajifunga’’ kwao wenyewe? ‘’ Naogopa hiki...’’ na ‘’ Nina wasiwasi kukusu hili..’’ ndivyo wanavyoongea.

Kipindi hiki,basi ni cha ubinafsi! Na kadri tunavyohusika na sisi wenyewe,ndivyo tunavyozidi kuogopa na nasfi yetu pia inaumia.Tunahofia yatakayotukia nafsi yetu.Mawazo yetu yasiyoelekezwa yanaengaenga na kuyaedekeza nafsi.

Kwa namna nyingi hisia isiyoelekezwa ya hofu inatuongoza kwa matokeo ya hatari-ya kukosa tumaini.Kuna hofu kwamba ‘’kuna kitu kibaya kwa ubongo’’-kwamba kuchanganyikiwa akili inakaribia,kwamba wazimu unaweza kutokea.

Kwa namna nyingine hisia isiyoelekezwa inaleta kutojiamini ama udhalili,upungufu wa kiakili,upungufu wa kiume.Hofu moja inaongoza kwa nyingine mpaka mtazamo wa kiakili na afya yetu inaharibika daima!Lakini kuna njia ya kurekebisha shida hii.Kuna njia ya kushinda hofu!

**Je,Hofu Zote ni Vibaya?**

Kwa muda wa millennia/miaka elfu shida ya hofu imekabiliana na kutatanisha wafikiriaji wetu wakuu.Wanafilosofia hawajapata suluhisho la kutosha-ama maisha yao hayangevunja mioyo kila mara! Wanasaikolojia wameleta dhana ya pendekezo lenyewe kama suluhisho la kushinda hofu.Wale waliojaribu mbinu hii bado wamepatikana kukosa raha ya kiroho.Bila shaka! Kwa pendekezo lenyewe ni njia ya ujanja ya kujidanganya! Na udanganyifu hausuluhishi chochote.

Wengine wamejaribu vitulizi kupunguza hofu yao ya kiakili.Vidonge vingi kutuliza neva na kumfanya watu wafurahi vimeuzwa na wauzaji dawa na madaktari.Lakini hofu na wasiwasi na magonjwa ya mwili na akili bado yanaongezeka!

Ili tufike suluhisho lazima tugundue aina MBILI ya hofu:1) hofu ya manufaa na 2) hofu ya madhara.Bila hofu ya kawaida,ya manufaa hakuna mtu awezaye kuishi leo hii!Hofu ifaayo inaongoza kwenye ulinzi wa kibinafsi.Bila hofu hii hatuwezi kufanya mazoezi yafaayo ya tahadhari dhidi ya jeraha.Hiyo ndiyo aina ya hofu tunayohitaji!

Lakini kumbuka! Wakati wazo letu halijaamuriwa vizuri ,hofu ya kawaida ya kujilinda inageuzwa kwenye hofu yasio ya kawaida ya kulinda NAFSI.

**Hofu ni Kitu cha KUFUNZWA**

Kudhibiti jazba ya hofu ni mchakato tunaojifunza-ni jambo la elimu.Inahitajika tujifundishe kuhusu hofu inayofaa.Alafu tufanye jinsi mwafaka ya kudhibiti hofu hiyo.Lakini ni lazima tuepukane na hofu ya madhara na yasiyo na mwelekeo.

Hofu inayostahili ni hekima.Pia ni maarifa.Tuseme,kwa muda mfupi,tumekabiliana na hatari halisi.Ni kawaida kuwa na hofu.Lakini inatakikana tudhibiti hofu yetu.Hofu inatueleza kwamba kuna kiti kibaya.Inatuonya kwamba ni lazima tukabiliane na hatari zetu kwa njia ya utulivu na uangalifu.Lazima tushughulike na kuchukua HATUA.Hatua inasuluhisha hatari! Lakini kwa kuweka wasiwasi juu ya shida na kuogopa kwamba mabaya zaidi yatafanyika haitatusaidia.

Watu wenye wasiwasi sugu ambao wana hofu nyingi,mara nyingi ni wasukumaji wa mambo na wasioweza kufanya uamuzi.Wanaogopa kuchukua hatua.Hofu inakuwa kiongozi wao.Wanakuwa watumwa wa hofu.

Wakati wa kujifundisha kumudu hofu yetu ni wakati tu wachanga-na bado MWELEKEO HALISI YA MAWAZO KATIKA MIAKA HII YA AWALI HAUFUNDISHWI NYUMBANI AU SHULENI!

Lakini haujachelewa sana kufundishwa.Maisha ni bora sana kwetu kuliko kubaki katika kutojali,haijalishi hata kama tumezeeka.Wacha tujifunze KUTOFAUTISHA kati ya hofu yanayofaa na ya madhara.

**Hofu na Woga usiohitajika**

Wakati mwingine hofu yetu ni duni sana na hata inazua kicheko-kwa mtu mwingine,kwa hakika.Hapa ndipo baadhi ya hofu duni ambayo inapiga watu:hofu ya mafuriko ya maji,hofu ya usafiri wa ndege,hofu ya ukimya,giza,kivuli kutoka kwa mbalamwezi,hofu ya simu,telegramu,vibyongo na panya!

Hofu hizi mara nyingi ni matokeo ya sehemu ya uzoefu ambao tumeruhusu kutusumbua aidha kwa kufahamu au bila kufahamu.

Mara nyingi kwa hali mbaya sana ni woga wa kawaida ambao unaumiza watu kwa njia isiyo ya kawaida.Hofu ya mahali pa damu,hofu ya mnyama,hofu ya upweke,HOFU YA UMBO LISILOVUTIA,HOFU YA KUWA MWOGA na HOFU YA KUSHINDWA.Kwenye orodha hii twaweza kuongeza hofu ya kila kitu,tabia ya mtu anayeepuka maisha!

Kwa msingi ya hofu hizi zisizo za kawaida kuna hofu za kawaida.Lakini kwa kila namna hofu ya kawaida imeruhusiwa KUTOKA NJE YA UDHIBITI.Shuhudia idadi ya mamilioni ya wasichana na wanawake ambao wameogopa kwamba wanaweza kuona umbo lisilofaa au wameona.Jeraha ya hatari ya kiakili,kimwili na kihisia imefanywa mara nyingi ''kuondoa'' hofu hizi.Hali hatari inasababisha hofu zaidi.Mzunguko usio wa kawaida unatokea.

Je,umewahi kujua watu ambao walikuwa na hofu ya kuogopa? Hawawezi kueleza hofu yao,lakini wanajua kitu cha hofu kinaweza kuwatokea! Hawajafunzwa somo la maisha ambalo hofu yetu ya hatari na uzoefu HAUJAWAHI KUTOKEA!

Wakati mwingine,hata hivyo,tunajiletea hofu na wasiwasi kwetu wenyewe.Ayubu aliandika: ''Maana ni jambo hilo nichalo hunipata,Nalo linitialo hofu hunijilia.'' (Ayubu 3:25).Wanaume na wanawake wengi wenye uwezo wamepata kushindwa kwa kujitoa kwa hofu isiyo na mwelekeo ya KUTOFAULU.Haswa jambo hili limekuwa la kweli tangia vita vya ulimwengu na maangamizi ya majonzi.Hofu hii imesababisha HOFU YA KUKOSA USALAMA.Kumbuka jinsi wasiwasi moja inalea nyingine.Hofu hizi na tabia ya kukosa maarifa ya hekima.

KINACHOSABABISHA hofu hizi zisizofaa kinaegemea katika utambuzi pungufu na udhibiti wa shida za hisia ambazo tunakabiliana nazo tunapokomaa.Wazazi wajeuri,kina baba wasiojali,kina mama wanao tabia ya kumiliki zaidi,chuki za familia na mababu wanaohangaika-hawa wanasababisha wingi wa shida zetu za hisia.Lakini kimsingi KINACHOSABABISHA hofu ZETU ni kushindwa KWETU kutambua na kusuluhisha shida hizi za hisia.

**Mfano wa Kawaida**

Hapa ni mfano wa matokeo yanayosababishwa na kushindwa kuadhibu hisia zetu za akili.Msichana mdogo amehusishwa katika ndoa.Badala ya kufurahi,anavunjwa na migogoro na hofu.Anatishwa na majukumu ya maisha ya ndoa na uzazi.Kuchanganyikiwa kiakili kunaonekana hakuepukiki.Kwa nini?

Kawaida katika usuli wake utapata baba asiye na mawazo,mama aliyekata tamaa,walimu waseja,hamna mwandani wa rika yake akiwa balehe.Shida za kiakili zisiposuluhishwa zinaleta usumbufu wa kimwili.Kuvunja ungo si ya kawaida na mara nyingi ya maumivu.Hofu ya kuzaa unamsumbua kwa sababu ya hadithi ameisikia kutoka kwa ''marafiki''.Hili silo jambo la kipekee.Huu ni MFANO WA KAWAIDA.Wengi wenu wanateseka kutoka kwa shida kama hii.

Wacha tuelewe,sasa,kwa nini shida za hisia zaongoza kwenye shida za kimwili,kama vile ilivyotajwa.

Kuna uhusiano wa mawazo na mwili ndani ya kila mtu.Lazima tuongoze na kuratibisha mwili na mawazo kabla hatujafikisha furaha na kushinda hofu zetu.Suleimani alielewa shida hii wakati aliandika: ''Moyo ulio mzima ni uhai wa mwili;Bali husuda ni ubovu wa mifupa'' (Mithali 14:30).Na pia, ''Chakula cha mboga penye mapendano;ni bora kuliko ng'ombe aliyenona pamoja na kuchukiana.'' (Mithali 15:17).

Kuna uhusiano ya meng'enyo wa chakula na afya na wazo.Wakati wazo lina hofu,linatuma

ujumbe kwenye tezi mbalimbali na viungo ili viwe tayari kwa hatari.Viungo vinajaza mishipa ya damu na vifaa ili tuweze kuwa tayari kukutana na hatari.Wakati tunasongeza mambo na kukosa kufanya uamuzi,miili yetu inajaa na vifaa visivyotumika.Tezi zetu zinaondolewa kwa njia isiyofaa.Hofu ya kujichochea ya kila mara baadaye inasababisha tezi zifanye kazi kwa njia isiyo ya kawaida.Mwili mzima unateseka na kwa hivyo hulka na hata mawazo.

Hofu zisizoshindwa ndizo chanzo cha sehemu kubwa ya magonjwa.Kwa kweli,Mazoea yafaayo ya vyakula,mazoezi yafaayo na kuondoa pia ni sehemu muhimu katika afya-Kiakili na kimwili kijumla.

Wakati miili yetu imejaa sumu ambazo zingetumika katika utendaji wa kukabiliana na hatari kamili,tunajipata ''tumechoka'' na ''kuvurugika''.Watu mara nyingi husema, ''ni neva wangu.''Neva hazina shida.Tunazihitaji ili tuishi.Ni yale tunayoyafanyia neva ndiyo shida.Tumezichakaza kwa kuzitumia sana kutokana na wasiwasi isiyofaa na hofu.Tumegeuza utaratibu wa neva uliotengenezwa kwa ajili ya KULINDA NAFSI kuwa kifaa cha KUHARIBU NAFSI.

**Ndoto za Kuogofya**

Wakati tumeingiza machafuko ya mwili katika miili yetu,wazo linaanza kucheza shere ndani yetu.Ubunifu wetu unafaa utumike kuleta mawazo mapya na mazuri.Ni chombo cha maendeleo.Badala yake,tunaruhusu ubunifu wetu kututisha na mawazo mapya na HOFU za kuongezwa.Tunafikiria kwamba tunateseka kutokana na kuvimbiwa,baadaye twapata vidonda vya tumbo na saratani-na baadaye MAUTI,hofu kuu mno! Wakati mwingine tunafikiria kwamba tunateseka kutokana na kuchanganyikiwa kiakili ama upungufu wa akili.Maisha yanaanza kutisha.

NDOTO za kutisha zaanza kutuumiza.Ndoto nyingi zatoka kwenye matumizi zaidi ya mawazo.Mahangaiko ya kila siku yanatuweka chini tunapopumzika usiku.Hatujui kuburudika.Suleimani alisema: ''Kwa sababu ndoto huja kwa sababu ya shughuli nyingi,' (Mhubiri 5:3).

Kwa vile shughuli za utambuzi ambayo watu wengi wamebanwa nayo ni ile ya kutengeneza hofu na wasiwasi mpya,ndiyo maana mshangao ni kwamba damu inayoenda kwa pupa itatengeneza hofu katika NDOTO?

Wakati hali ya wasiwasi wa akili inachukua muundo mbaya,ndoto na jakamoyo zinajenga HOFU YA KIFO-na mara nyingi husababisha kifo kabla ya wakati.WALIMWENGU WENGI wamekuwa watumwa wa hofu ya kutisha! Hofu hii inavunja usawa wa akili na kuharibu mwili.Inasababisha uelewaji mbaya wa kiroho ambao wakati mwingine wanajiweka katika dhuluma ya kidini.Dhuluma ni vali inayokomboa kukataa tamaa iliyogandamizwa kiroho,hofu,na hisia ya kujilaumu.Lakini dhuluma haina suluhisho kwa shida.

**Njia ya Kuepuka Hofu**

Mradi tu tumegundua hofu hizi ambazo twahitaji kupigana nazo,inabidi tutafute njia mwafaka ya KUUTEKA shida hizi.Kujidanganya kisaikolojia hakutasaidia.Hakuna mema kwa kusema kwamba kifo siyo adui wetu-kwamba ni rafiki mema.Uamuzi huo wa juu juu haubadilishi hakika kwamba kifo ni adui wetu.Njia ya kusuhisha hofu hii-na kusuluhisha hofu yoyote isiyohitajika-ni kugundua kiini chake.

Paulo anatueleza kwamba mauti ni uadui (1 Wakorintho 15:26).Lakini Yesu Kristo alitengeneza njia ya kuepuka adhabu zake za milele. ''Mwokozi wetu Kristo Yesu...aliyebatili mauti na kuufunua uzima na kutokuharibikia,kwa ile injili.'' Maana Mungu hakutupa roho ya woga,bali ya nguvu na ya

upendo na  ya moyo wa kiasi.'' (II Timotheo 1:10,7,tafsiri ya Panin.

**Lakini tunapotesaje woga wa kifo-na hofu zote zingine na wasiwasi ambazo zinatuingilia?**

Kumbuka  tulijifunza katika somo la kwanza kwamba tunahitaji kugundua tofauti kati ya hofu ya manufaa na ya madhara,hofu isiyozuiliwa.Hofu inaweza kuwa mzuri au mbaya kulingana na mwelekeo ya hisia.Hofu halisi inatoka kwenye mvuto wa kujilinda.Inaonyesha hatari-adhimisha kwamba inafaa tuchukue HATUA.

Hofu halisi ni aina mbili.Ya kwanza ni woga ya kawaida ya hatari-onyo kwamba twahitaji kulinda maisha yetu.Nyingine ni WOGA WA KIROHO ya kujilinda milele.Watu hawatambui woga huu.Na bila woga huo,hatutaweza KUUTEKA hofu isiyodhibitika.

Woga huu wa KIROHO unaitwa KUMCHA BWANA ama KUMCHA MUNGU.Kama vile hofu nyingine,hofu hii pia imeelekezwa vibaya mpaka imekuwa hofu ya shetani.

Hisia ya kawaida ya hofu ya kimwili inatuonya kuhusu hatari za kimwili.Hii ni hofu ya kufundishwa.KUMCHA MUNGU inatuonya dhidi ya hatari za milele.Hofu hii pia ni ya kufundishwa.Inatubidi tujifunze kuhusu nguvu na mamlaka ya Mungu.Tunajifunza ya kwamba Mungu ndiye mpaji wa uhai na pia Yeye ndiye anachukua uhai.Ndiyo maana Yesu alisema: ''mwogopeni YULE (Luka 12:5).

**Kwa Nini Kumcha Mungu ni wa Muhimu**?

Kizazi hiki kimepoteza heshima ilio hai kwa Mungu.Kumbuka mfano wa Nuhu: ''Kwa imani Nuhu akiisha kuonywa na Mungu katika habari za mambo yasioonekana bado,kwa jinsi alivyomcha Mungu,aliunda safina,apate kuokoa nyumba yake,'' (Waebrania 11:7).Nuhu aliogopa nguvu za Mungu.Huu ni uwoga mzuri,woga halisi wa Mungu.Hakuacha hofu yake ilete wasiwasi na kuvunjika moyo.Nuhu ALITENDA kulingana na hofu yake.Alifanyia kitendo hofu yake!

Umuhimu mkuu wa KUMCHA MUNGU haujaleweka kihuzini.Wacha tuelewe umuhimu wake kamili. ''Kumcha Bwana ni maonyo ya hekima'' (Mithali 15:33).

Tukimcha Mungu,tunaheshimu anayosema.Anayosema imeandikwa katika Neno Lake,Biblia.Ndani ya Biblia mna hekima ya Mungu.Maagizo yake yatueleza mema na mabaya.Yanatufafanulia hatari za dhambi.Yanatuonya dhidi ya hatari ya maovu ambayo yanatunyima raha na Baraka na uzima wa milele. ''Kumcha BWANA huelekea uhai;Atakaa ameshiba;hatajiliwa na ubaya.''(Mithali 19:23)

Uhitaji wa kumcha Bwana ni fundisho la Agano Jipya.Petro alisema: ''Mcheni Mungu'' (1 Petro 2:17).Pia imerudiwa katika  Ufunuo 14:7: ''Mcheni Mungu.''Kanisa la Mungu la awali lilikuwa na amani wakati ''likiendelea na kuongezeka katika kicho cha Bwana,na faraja ya Roho Mtakatifu'' (Matendo 9:31).

**Jinsi ya KUCHUKUA HATUA ya Kumcha Mungu**

Ni jinsi gani ITIKIO kamili ya kumcha Mungu itatuondolea mateso ya kiakili yasiofaa ambayo tunalazimisha kwetu? Ni jinsi gani kumcha Mungu itatufundisha kudhibiti na kuelekeza mawazo yetu mpaka tuuteke kila hofu ya neva?

Mtume Yohana aliandika: ''Katika pendo hamna hofu;lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu,kwa maana hofu ina adhabu;na mwenye hofu hakukamilishwi katika pendo'' (1 Yohana 4:18).

Wasiwasi na sononeko ya kiakili inayotokana na hofu inafanyika  wakati UPENDO

haujakamilishwa.UPENDO ni kufanya analoamuru Mungu: ''Kwa maana huko ndiko kumpenda Mungu,kwamba tuzishike amri zake;wala amri zake si nzito'' (1 Yohana 5:3).

Amri za Mungu zinafafanua mema na mabaya.Zinatueleza hatari za dhambi ''dhambi ni uasi'' (1 Yohana 3:4)Kwa KUMTII Mungu tunaepukana na hatari ya maovu na tunajaza mawazo yetu na hisia zetu na UPENDO.Upendo unaondoa wasiwasi na sononeko.Hiyo ndiyo jinsi ya kuchukua hatua kwa kumcha Mungu.

Basi wacha tujifunze KUPATA UPENDO KAMILI.Petro husema hivi: ''Naam,kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu,katika imani yenu tieni na wema,na katika wema wenu maarifa,na katika maarifa yenu kiasi,na katika kiasi chenu saburi,na katika saburi yenu utauwa,na katika utauwa wenu upendano wa ndugu,na katika upendano wa ndugu,UPENDO'' (II Petro 1:5-7). (Neno la kale ''msaada'' linalopatikana katika KJV,linafaa liwe UPENDO).

HATUA SABA ambazo unapaswa kufuata ili ujiondoe kwenye hofu ni hizi!

Kwanza,kumbuka kuanza na imani.Imani ni nini? ''Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza;kwa mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko,na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao'' (Waebrania 11:6).

Huwezi KUMCHA Mungu pasipo imani kwamba Yeye yuko na anatupatia kulingana na tuliyofanya,iwapo ni mema au maovu.Imani si kitu unajaribu kujifanya kuwa nacho wakati huna.Imani ni kutambua kwamba Mungu yupo na kuwa ni hatari kuanguka katika mikono yake isipokuwa umegeuka toka kwa dhambi zako!Imani ni kitu cha kutafuta.Unafundishwa kutoka kwa uzoefu.Hauwezi kupumpaza akili  katika kupokea imani.

Huenda ikawa unafanana na mwanamke aliyeniandikia: ''Sioni nikijifanya kumcha Mungu.''Hakika huwezi  kujifanya kumcha Mungu! Lazima upate uzoefu wa kuhitaji kumcha Mungu.Pengine unapaswa kuwa msomaji wa kila siku ya jarida la UKWELI WAZI kujifunza mamlaka na nguvu ya Mungu!

Wacha tufuate maagizo ya Petro katika mpango wake saba ya kushinda hofu kwa kujaza mawazo na UPENDO.

**HATUA SABA ZA MPANGO**

Kwanza,tia wema kwenye imani yako katika nguvu za Mungu.Wema unamaanisha ustahifu,sahili,wastani na tabia njema.Ni kinyume cha matusi na ushenzi.Hatua ya kwanza ni kuondoa chanzo cha kujilaumu,dhambi za siri  ambazo zinatendwa kwa kusingizia adabu mno!

Inalazimu tuwachie Biblia ifafanue ustahifu,usahili na tabia mema.Soma maisha ya wanaume na wanawake ambao yameandikwa katika kurasa zake.Tambua makosa yao.Usirudie makosa hayo.Kumbuka,pia ,kwamba kumcha Mungu inatufundisha kwamba tusiweke mawazo yetu vile tunataka kuamini,lakini kuamini na kufanya vyema jinsi Mungu alisema.Siyo Kujifanya mwenye haki ama kutamka matusi.Ni ustaarabu halisi.

Ya pili,tia maarifa kwenye wema.Maarifa yamaanisha kujifundisha mawazo na kanuni za mwenendo.Lazima tuongeze maarifa kila mara mpaka tusafishe tabia zetu!

Ya tatu,tia maarifa kwenye kiasi.Tukijifunza kwamba Mungu anaturuhusu tutumie vitu ambavyo tulikatazwa tusitumie,inafaa tuwe na kiasi katika kutumia uhuru wetu mpya.Ni lazimu tuwe na kiasi.Kiasi hakimaanishi kizuizi.Kizuizi ni kutokuwapo kwa kitu/jambo. Kiasi ni utumuzi wa kawaida! Paulo alisema: ''Na kila ashindanaye katika michezo hujizuia

katika yote'' (1 Wakorintho 9:25).Kiasi humaanisha KUJIHAKIKI.Hii ni hatua muhimu sana ya kudhibiti mawazo na hofu zinazochipuka.Unahitaji ufanye zoezi la kujiwekea nidhamu juu ya mawazo na mwili ikiwa unataka kushinda hofu.

Ya nne,tia saburi kwenye kiasi.Saburi ni ile upana wa mawazo ambapo unangojea matokeo kufanikisha.Saburi ni kinyume cha wasiwasi.Aliye na saburi hawezi kufadhaika kwa sababu shida haziwezi kupata suluhisho mara moja.Saburi inatokea kwa kufanya mazoezi ya kujihakiki ukiwa katika jaribio. ''Dhiki kazi yake ni kuleta saburi,'' Paulo aliandika katika (Warumi 5:3).Huwezi kukaa chini na kujitengenezea saburi.Lazima ufanye bidii kuipata saburi katika majaribio!

Ya tano,tia utauwa kwenye saburi.Utauwa unamaanisha kuwa na kama Mungu katika tabia.,Mungu amefafanua tabia zake katika Biblia mzima. ''Walokole'' wengi wajifanya watauwa,huku wakikana NGUVU za Mungu '' (II Timotheo 3:5).Mungu ni mhusika mwenye nguvu,si mdhaifu.Utauwa unaamanisha nguvu katika tabia-inajumlisha wema,maarifa,saburi,kiasi.Watu wengi wanajaribu kufikiria jinsi Mungu alivyo bila kusoma maandiko.Wachache wanastaajabu kwamba wamekana nguvu zake Mungu!

Ya sita,tia upendano wa ndugu kwenye utauwa.Ni rahisi kujifanya mtauwa kuliko kumjali ndugu yako! Yakobo anaeleza kuhusu ulimi wa mwanadamu: ''Kwa huo twahimidi Mungu Baba yetu,na kwa huo twalaani wanadamu waliofanywa kwa mfano wa Mungu.''(Yakobo 3:9).Mungu ni mkamilifu.Inafaa tuwe wakamilifu.Lakini ndugu zetu wana udhaifu wa kimwili.Ni vigumu kumjali,kumsaidia,kuwa mkarimu,kuwa mkali kwa lazima kwa mwenzio.

Katika ghera inayopotosha wengi wanalazimisha ''wema'' wao kwa wengine.Inafaa tujifundishe uamuzi mwema katika kuwa wema.Kwa upande mwingine,wengi wanapuuzia wema,ambao hawawezi kuutengeneza.Hii hulea huzuni na wasiwasi.

Ya saba,tia UPENDO kama upeo wa utimilifu.Yesu alisema: ''Wapendeni adui zenu,waombeeni wanaowaudhi'' (Mathayo 5:44).Ukipenda maadui wako kiasi hicho.hautahofia watakachokufanyia.Upendo ukikamilishwa huondoa hofu zote! Yesu pia alisema: ''Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu,wa mtu kuutoauhai wake kwa ajili ya rafiki zake.'' (Yohana 15:13).Upendo kamili huondoa hata hatari mbaya sana-hofu ya kifo!

**UPENDO ni Nini?**

Upendo ni utimilifu wa sheria ya Mungu kulingana na roho na dhamira: ''Pendo halimfanyii jirani neno baya;basi pendo ndilo utimilifu wa sheria. (Warumi 13:10).Huwezi kumpenda mtu bila kutimiza sheria.Na huwezi kutimiza sheria kamili bila kumpenda jirani na adui wako! Upendo unajumlisha dhamira ya roho na sheria ya Mungu.Ni jumla ya mambo yote mema na mabaya.Kumcha Mungu kunaleta upendo.

Kumbuka vile andiko linafafanua upendo kinagaubaga. (Katika mistari inayofuata neno la kizamani ''msaada'' linatakikana lifasiriwe UPENDO,ambalo nimefanya): ''Tena nikitooa mali zangu zote kuwalisha maskini,tena nikijitoa mwili wangu niungue moto,kama sina upendo,hainifaidii kitu.''...Ukarimu wa ndugu bila UPENDO haufaidii chochote kamwe! ''Upendo huvumilia''-hufadhili;upendo hausuhudu-''upendo hautakabari''-;haujivunii,haukosi kuwa na adabu''-hautafuti mambo yake-''hauoni uchungu;hauhesabu mabaya-haufurahii udhalimu,bali hufurahi pamoja na kweli''-Huvumilia yote;huamini


yote''-''hutumaini yote;hustahimili yote.- ''Upendo haupungukiwi neno wakati wowote''- bali ukiwapo unabii utabatilika,zikiwapo lugha,zitakoma,yakiwapo maarifa,yatabatilika''

Upendo HAUBATILIKI: (I Wakorintho 13:3-8).

Hivi ndivyo utakavyoshinda hofu zako na wasiwasi! Omba Mungu usaidizi kutekeleza mipango yake saba ili upate amani kamili ya mawazo. '' Ombeni,nanyi mtapewa'' (Luka 11:9).

**KOZI YA KUJIFUNZA BIBLIA**

Somo la 11:**Rekodi Katika Jiwe**




Bob Thiel,Mhariri Mkuu
Imechapishwa 2017 na Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG)

Kozi hii inatokana kwa kiwango kikubwa na kozi kwa Mawasiliano iliyohaririwa mwaka wa 1954,iliyoanza chini ya usimamizi wa hayati C.Paul Meredith kupitia Kanisa la Mungu la Redio.Baadhi ya maeneo yake yameboreshwa ili yaendane na karne ya 21 (japo mengi ya maandishi ya awali yamebaki yalivyo).Kadhalika imeongezewa vifungu toka Maandiko Matakatifu,pamoja na taarifa na maswali ambayo hayakuwemo katika kozi ya awali.

**UUMBAJI UNATHIBITISHA UKWELI WA BIBLIA**

BIBLIA YAKO humaanisha hasa inayosema.Taarifa zake za UKWELI ni HALISI.Wakati wowote ishara imetumika,INAFAFANULIWA katika maandiko.

Lakini walimwengu hawaamini Biblia.Hata viongozi wengi wa makanisa hawaamini hakika yake.

Na bado ni ukweli-tena UNATHIBITISHWA! Watu wengi mara nyingi wanatugutia kwa mshangao wakisema, ''Kwa nini unachukua yaliyosemwa katika Biblia KIHALISI TU!'' Siku

hizi watu aidha wanaamini kuwa Biblia haimaanishi vile imeandikwa kwa hivyo MUNGU HAMAANISHI ANACHOSEMA;ama watu wameongozwa KUTOAMINI Biblia mzima na KUKANA UKWELI KWAMBA MUNGU YUPO!

Ni wakati ambapo panatakikana tujue UKWELI kuhusu MAMLAKA ya Biblia!

**Nyakati za Hatari Mbeleni!**

Matukio ya mwisho wa nyakati hizi yanapangika kwa upesi mno.Katika upeo wa janga linalokuja hivi karibuni,inatakikana kuamini Mungu kwa uthabiti.NYAKATI ZA HATARI ZI MBELENI.Lakini Kristo aliahidi, '' Lakini ATAKAYEAMINI hadi mwisho,ndiye ATAKAYEOKOKA'' (Mathayo 24:13).

Thibitisha peke yako sasa-KABLA YA DHIKI KUU-Kwamba MUNGU YUPO na ANAMAANISHA ANACHOSEMA.

Inatakikana uwe na imani  thabiti kwamba BIBLIA NI YA KUTEGEMEWA! Inafaa UJUE-NA KUJUA kuwa unafahamu-kwamba Biblia ni mwongozo mtakatifu,maarifa ya muhimu ya Mwenyezi Mungu kwa wanadamu! Kwamba unafuata njia IFAAYO wakati UNAYATII MAAGIZO YA MUNGU AMBAYO YANAPATIKANA KATIKA BIBLIA-maagizo ambayo yatawezesha kufika kwenye wokovu katika hizi nyakati za hatari!

**Sayansi Kuenda Mrama**

Mtume Paulo anaonya dhidi ya UPINZANI ambao ''Sayansi'' inadokeza dhidi ya kuchukua Neno la Mungu-Biblia-kuwa HALISI.Kwa hivyo anasema, ''...ujiepushe na maneno yasiyo ya dini,yasiyo ya maana,na mashindano ya elimu iitwayo elimu kwa uongo ambayo wengine wakiikiri hiyo wameikosa Imani...'' (I Timotheo 6:20-21).

Sayansi ya Mageuzi inakana Neno la Mungu lililofunuliwa ambalo laeleza kwamba ALIUMBA ulimwengu pote.Inapatikana katika Nadharia ya Mageuzi ambayo inakana THIBITISHO Kuwa Mungu ni MWUMBAJI,na inakana MAELEZO YALIYO WAZI ya Biblia kuhusu asili na historia ya dunia.Lakini wanasayansi WANAPUUZIA haya bila THIBITISHO LA KISAYANSI ambalo wanadai kwenye maswali ya kawaida.Umefika wakati ambapo twafaa TUACHE KUPUUZIA-ni wakati ambapo tunapaswa KUHAKIKISHA MAMBO YOTE! (I Wathesalonike 5:21).

THIBITISHO LIFAALO la kuwepo kwa Mungu na mwongozo takatifu ya Biblia ni pana,na unajumuisha yote,ni anuwai katika mashinikizo yake,na ni vigumu kuweza KUKWARUZIA USO katika somo hili fupi!

Basi wacha tuanze somo hili la ajabu na tujue jinsi uumbaji wa Mungu unathibitisha ukweli wa Biblia.

**Somo la 11**

**Uumbaji Unahitaji Muumbaji**

Wanamageuzi,katika jaribio lao lenye ubatili wanahakiki kuwa Nadharia ya Mageuzi kila mara INALAZIMISHWA kuanza na utaratibu wa ulimwengu na KUWEPO KWA MATA.Nadharia ya Mageuzi YANAANZA na mata,sheria na uhai kidogo!

Lakini mata ni nini?

Mata ni chochote kimilikacho nafasi na kina uzito.Si lazima mata ionekane,kwa sababu gezi zingine,na hata hewa tunayopumua,pia inawekwa katika kundi la ''mata.'' Hata hivyo,uvumbuzi katika Fizikia ya nyuklia,na kupitia majaribio ya Madame Curie na radiamu,wanasayansi sasa wamegundua kwamba kuna kiasi cha ''uchangukaji'' katika mata! Kuzorota kwa mata ya mionzo ni hakika! Urani (U 238) polepole inaanza,kama unavyojua,ni mionzo na inatoa nishati aina ya kumeremeta.

Polepole baada ya miaka michache,vifaa vya mionzo vinasambaratika na vinakuwa risasi! HAMNA URANI UNAOKUWEPO KIKAWAIDA SIKU HIZI! Hii inamaanisha kuwa Sayansi IMETHIBITISHA kwamba dunia hii polepole inaendeshwa! Dunia na ulimwengu wote ni kama SAA kubwa ambayo kwa wakati mmoja ILINING'INIZWA! Na polepole inasonga tangia ining'inizwe haijulikani kwa mchakato wo wote ama kutazamwa ama kupimwa,ama kama itapandishwa tena!

Ni kama binadamu amefika kwenye eneo katikati ya mpangilio wa ulimwengu ambao polepole ''UNAENDESHWA.''

Sayansi imethibitisha,hapo awali,kwamba MATA HAIJAWAHI KUWEPO MILELE! (Wanasayansi wengine wamedai kwamba kuna kitu kiitwacho nadharia ya ''ulimwengu bembea'',(lakini imetiwa shaka na wengi wao).

Mata lazima kwa wakati mmoja IMEKUJA KUWEPO! Kwa vile mata,asili yake HAIJAKUWA NA UMILELE,lazima IMEANZISHWA ILI IWEPO!

Hapa mwanasayansi Mheshimiwa James Jeans anakubaliana na mwanzo wa mata. ''Kila kitu kinaashiria nguvu nyingi kwenye tukio la ajabu,ama mfululizo wa matukio YA UUMBAJI katika nyakati hizi sio dhahiri na unatengana mbali!

Ulimwengu HAUNGEJITOKEZA kibahati kutoka kwa viambato vyake vya kisasa,na pia haungekuwa vile ilivyo kwa wakati huu.''

UUMBAJI,halafu,KUWEPO KWA VITU,hakika UNATAKA na KUHITAJI MUUMBA! Kilichotengenezwa kinahitaji Mtengenezaji! Kile kilichobuniwa chahitaji Mbunifu!

Mata,vile imegunduliwa,IMETENGENEZWA-''haikujitokeza tu'' na haina umilele kwa wakati uliopita! Kwa hivyo,hapa tunaona uthibitisho ulio dhahiri kwamba VIUMBE VYOTE VYAHITAJI MUUMBAJI MKUU!

**MUNGU Ndiye Muumbaji**

**1.**Je,Mungu anaonyesha kwamba YEYE ndiye muumbaji wa vitu vyote? Mwanzo 1:1

**MAELEZO:**MANENO YA KWANZA MANNE unayosoma katika Biblia yako ni, ''Hapo mwanzo Mungu aliziumba...''! Mungu anakuonyesha kwamba YUPO.Hiki ndicho kitu cha kwanza anakueleza.Basi soma maneno mengine, ''aliziumba mbingu na nchi.''

Mungu anakuambia kwamba yeye ndiye Muumbaji! Chanzo kikuu ,ambaye ALIUMBA mata,anasimama akifunulia kama AKILI KUBWA na MUASISI WA VITU VYOTE!

Lakini Nadharia ya Mageuzi inayokubaliwa kote imetiwa kwa akili za watu,hata kiasi cha kujiuliza uthabiti wa ufunuo mkuu wa kwanza wa Mwenyezi Mungu!

Nadharia ya Mageuzi INAKUSUDIWA kukuongoza kufikiri ''kwamba Biblia siyo ukweli na HAIMAANISHI inayosema-kwamba kwa hakika HAKUNA Mungu kabisa!''

2.Ni nani anaye NGUVU HALISI nyuma ya maovu haya ya kufuta Mungu na Biblia kutoka kwenye akili ya watu? Ufunuo 12:9.

3.Je,kuna siku Mungu ATAKOMESHA Shetani asiwadanganye wanadamu? Ufunuo 20:1-3.

**MAELEZO:**Nadharia ya Mageuzi haitafundishwa kama ukweli katika Ulimwengu Unaokuja! Wakati Yesu Kristo atakaporudi duniani,wanadamu wote watajua ukweli kwamba MUNGU NDIYE MUUMBAJI MKUU WA VITU VYOTE!

**''Mageuzi'' ni Nini?**

Kabla hujaona thibitisho dhahiri na la ajabu kwamba Mungu pia ni MPAJI wa AJABU wa UHAI na kwamba rekodi yake ya kibiblia ya

MWANZO wa maisha ni ukweli,ni muhimu sana kufafanua,kwa urahisi maana ya neno ''mageuzi.''

Bila shaka,kuna mifuatano mingi inayoitwa ''mageuzi''.Mfuatano wa kukuza muziki kutoka kwa njia rahisi hadi njia ngumu kwa maana fulani ni mfuatano wa ''mageuzi''.Hii ni ukweli katika ubunifu wote wa kiteknolojia,hii pengine imefanya watu wengi WAMECHUKUA kwamba maendeleo haya pia una ukweli katika vifaa VILIVYO HAI!

Hapa,imesemwa kwa urahisi,ni DHANA YA KIMSINGI ya Nadharia ya Mageuzi: ''Mageuzi ni kustawi polepole kutoka kwenye kitu chepesi,kwa hali isiyo na mpango ya asili ya awali hadi muundo wa utata wa maumbile ya ulimwengu,na pia kwa njia nyingine,kutoka kwenye mwanzo wa kiumbe hai wa sayari inayo uwezo wa kukuza maisha,kujitokeza na kuenea kwenye mifumo yote tofauti ya viumbe vinavyoanzisha falme za wanyama na miti''. ( ''Organic Evolution'',Lull,p.6).

Hebu kumbuka! Mageuzi inaongea kinadharia KUTOKA MWANZO WA KIUMBE HAI-tayari kinacho UHAI wa kuanzia! Sasa hayaonyeshi,ama hayajawai kuonyesha,na hayataonyesha jinsi uhai ULIKUJA kuwepo!

Nadharia ya Mageuzi (neno ''nadharia'' linamaanisha ''TUNAFIKIRI'') inaeleza kwa urahisi,kwamba mifumo yote ya uhai ambayo twajua leo hii,hata ya binadamu,miti yote na uhai wa wanyama katika jamii elfu,WAMEFUKA kutoka kwenye mfumo rahisi sana hadi maisha magumu,yenye kutatanisha na jamii zinazotegemeana ama ''asili,'' ambao tunaona leo hii,kila kiumbe kina tabia inayobadilika na ya kipekee,kila kiumbe kinazaa kulingana na asili yao.

Mageuzi yanaeleza kwamba uhai umegeuka kutoka kwenye mfumo wa polepole na '' NGUVU ZA KIENYEJI'' hadi maisha magumu ya leo.

Na hapa ndani,kwenye SHINA LA MTI la mawazo yote ya kimageuzi,inapatikana THIBITISHO KUU la Mungu na msukumo wa kiroho wa Biblia!

**Sheria ya Mwanzouhai**

Kuna sheria dhahiri inayodumisha thibitisho la kuwepo kwa Mungu awapaye uhai (1 Timotheo 6:13).

Hii ni sheria ya Sayansi ya Biogenesis!

''Bio;; inamaanisha uhai. ''Genesis'' inamaanisha mwanzo.Sheria hii,basi ni sheria inayohusu MWANZO wa uhai.Sheria hii ikielezwa kwa njia rahisi,ni sheria halisi kwamba UHAI WATOKA KWENYE UHAI PEKEE (BIOLOGY,Villee,p.18).Kwamba kisicho na uhai HAKIWEZI kuzaa ama kuzalisha kilicho na uhai.Pengine hakuna sheria inayojulikana kwa Sayansi ambayo inaweza KUONYESHWA kama sheria ya Mwanzouhai.

Sayansi kitambo iliamini nadharia hafifu ya ''kizazi huria''...kwamba uhai ulichipuka kutoka kwenye kiumbe kisicho na uhai.Aristotle,mfano halisi ambaye ulimwengu wa zamani kote walipata kujua kuhusu Sayansi ya kawaida,alifundisha kwamba mfumo wa chini wa uhai ulichipuka hapo kwa hapo kutoka kwenye vifaa VILYOKUFA,visivyo na uhai.

Kulingana na Aristotle,buu wa nyuki ama nyigu,kupe,vimulimuli na wadudu wengine wengi walitoka kwenye umande wa asubuhi,ama walitoka kwenye kuni iliyokauka,nywele,jasho na nyama.'' (The Origin of Life'' A.I.Oparin,p.6).

Aristotle anadai kwamba minyoo walitoka kwenye unyevu.''Binadamu,'' Aristotle alivyofikira, ''wanaweza kuwa na chanzo sawia na minyoo.'' Alikanusha kwamba uhai unaweza kutoka kwenye uhai! Ubashiri huu wa ubatili wa Aristotle,na ujinga

huu,ulikubaliwa kama ukweli na wengi katika karne nyingi!

Katika mwaka wa 1668,Mtaliano,Redi,alichukua hatua ya kwanza muhimu ya kupinga dhana hii ya kizamani ya kipagani.Kwa kuweka chichi juu ya kopo la nyama,akawazuia nzi wasitage mayai kwenye nyama.Baadaye aliwazuia kutagaa kwa mabuu,ambao watu walidanganya kuamini kwamba wanachipuka PAPO KWA HAPO kama ''uhai mpya'' kutoka kwenye kifaa kilichokufa.

Baada ya darubini kuvumbuliwa mwaka wa 1683,kazi ya Tyndall na Louis Pasteur ilidhibitisha mwishowe kwamba ''sheria ya Mwanzouhai'' ilikuwa na ukweli kwa mifumo MIDOGO sana ya uhai pia.

Bado,wanamageuzi kimsingi waliamini katika Abiojenetiki,dhana kwamba kitu kisichokuwa na uhai zamani,kinaweza kuwa na uhai bila nguvu za kipekee za Mungu.

Wanamageuzi,wanajenetiki,wanabiolojia na wanasayansi ye yote katika Nyanja zote,hawajawahi kuonyesha,ama kutoa ushahidi mdogo kwamba VINAVYOISHI vyaweza kutoka kwa VISIVYOISHI!

George Wald,Profesa ya Biolojia kutoka Harvard alikiri:

> Mtu anafaa kutafakari ukubwa wa jukumu ili akubali kizazi cha huria ya viumbe vyenye uhai kuwa HAVIWEZEKANI.Bado hapo tunaamini kwenye kizazi cha huria .(The Physics of Life,p.9).

Kumbuka kwamba wanasayansi wengine bado wamezama katika Nadharia ya Mageuzi,hawawezi kujileta kwa kukubali thibitisho lisilopingika ya majaribio ya Sayansi ya maabara.

Ni ukweli kwamba majaribio mengine ya maabara yamefanywa ambapo ''viini vilivyodhaniwa vimekufa'' vinasemekana kuwa ''vimefufuliwa'' na kuvifanywa hai kwa njia ya mchanganyiko wa kemikali.Kauli hii,hata hivyo,ni MBALI SANA na '' kizazi huria'' ama abiojenesisi!

**Mafuatano Yasiowezekana**!

Hata kama tungeruhusu uwezekano wa huria duni ya uhai kwamba ilifanyika,ni nini ingejitokeza?

Uhai duni ungekufa.

Sehemu ya sababu hii ni kwamba hata seli moja ni tata,na hata hivyo ina mifumo midogo mbalimbali ya kibiolojia,hivyo wanasayansi wamepata kwamba mifumo mingi kimsingi ni muhimu kwa uhai kuwepo ama kuendelea.Wanasayansi wanatambua kuwa viumbe vilivyo hai lazima wawe na nafsi yao.wanapaswa kula na kuzi kuwepo.

Kimsingi kuna aina mbili za seli,prokoryoti na ukaryoti.Prokoryoti haswa ni vimelea lakini ukaryoti ni karibu kila kitu kingine.Zote hizo zina utando,ribosomu,mishipa ya mmeng'enyo na DNA zenye viini.Ukaryoti zina asidi ya amino 21,na zote zinatakikana ziwe katika maeneo yanayofaa na katika uwiano unaofaa ili uhai uwepo.Asidi ya amino/protini zinazopangana kwa hiari (na vitu vingine vinavyojitokea kisadfa hapo) vinaweza kufa kwa sababu zifuatazo:

1.) Viumbehai vyote vinahitaji miundo ya kibiolojia kama vile oganeli na utando.Ndani ya utando wao wana seli za ndani vipengele mumunyifu wa maji.Bila muundo wa utando/protini hatimaye zinaweza kuenea na kuharibu viumbehai.Viumbehai lazima kwa kiasi fulani wawe na nafsi.
2.) Viumbehai vyote vinahitaji chakula na mwelekeo.Kisicho na mpangilio

hakingetengeneza muundo wa kibiolojia unavyojulikana kama DNA-inayobeba viini (ama inayolingana nayo lakini duni),seli ingekufa.Hata kama ingekuwa na aina nyingine ya viini vingekuja kuwepo na uwezo wa kuamua vinavyokula na jinsi ya kupata chakula,pia hiyo haiwezekani.

3.) Protini haziwezi kuishi bila DNA na DNA haiwezi kuwepo bila protini,kwa hivyo hakuna njia kwamba zilifanyika kwa wakati mmoja.
4.) Hata kama seli ingekuwa na vitu vyote vilivyotajwa hapo juu,na protini sawia na DNA,bado ingekufa kwa sababu haingekuwa na haja ya kujitokeza ghafla kwa mfumo wa mmeng'enyo ili itumie chakula.
5.) Hata kama wanamageuzi wangepewa yasiyowezekana yote yanayojadiliwa kwenye makala hii,uhai duni ungekufa kwa haraka  kwa sababu haungekuwa na haja yake kujitokeza kwa ghafla na uwezo wa kuzaliana,wala haungekuwa na uwezo wa kiasili wa kufanya hivyo.

Hebu tuangalie tena katika njia nyingine tofauti kiasi.

Ikiwa asidi ya amino zote zingejipanga (hata kama haiwezekani hivyo),hazingekuwa hai.Ikiwa seli duni ingekuwa hai kidogo,ingekufa.Kwa nini? Kwa sababu seli zina viini vya ndani vinavyo vipengele mumunyifu kwenye maji na vinaweza kutokomea/kuharibika bila utando.Kwa hivyo haiwezi kuendelea mbele ya hatua hii.

Kama seli hii ingekuwa na utando,ni nini ingefanyika baadaye? Ingekufa.Kwa nini? Kwa sababu haingekuwa na uwezo wa asili ya kuthibitisha ya kwamba inafaa ile chakula kwa vile haingetengenezwa na kiini cha uhai.Kiini-uhai ni sehemu ya seli inayobeba DNA na maagizo mengine.

Chukua kwamba inapatikana kama maji na inafanya kazi kama chakula,nini itafanyika? Itakufa.Kwa nini? Kwa sababu hayakujitokeza na uwezo wa mmeng'enyo,haiwezi kumeng'enya na kutumia chakula.Kwa hivyo kuzidi hatua hii haiwezekani.

Katika Biblia ndiko tumeambiwa kwamba wakati Mungu aliumba uhai,alikuwa na nia kwamba wazaane (Mwanzo 1:11,28,29).

Wazo la ''akili bunifu'' ya Aliye Mtakatifu ndiyo maelezo ambayo hayapingi maarifa ya kisayansi yanayothibitika-kwa sababu maelezo yote yanaleta kitu kinachokufa.

Protini haziwezi kuzaliana-zinahitaji DNA.DNA haiwezi kuwepo bila protini,na protini kuwepo bila DNA (Pietzsh J.Understanding the RNAissance.c.2003.http://www.nature.com/horizon/rna/background/understanding.html viewed 05/05/12).

DNA kimsingi haiwezi kufanya chochote peke yake,inahitaji protini.Je,mwanasayansi ye yote aliye na akili timamu anaweza kuamini kwamba alijitokeza kighafla na kujipata pamoja mzimamzima kwa wakati mmoja kwa uhai vile unavyojua uhai ulikuja kuwepo bila Mungu kuingia kati?

Jibu linapaswa kuwa wazi,HAPANA.

Vile ilivyotajwa awali,Mungu anatarajia binadamu kumtambua kwamba yupo kwa kupitia masuala mbalimbali ya uumbaji wake (Warumi 1:20).Na kwa vile uhai haungejitokeza ovyoovyo,kuliwa na kuzaliana,Mungu pekee ndiye angeweza kuanzisha uhai.Na hayo ndiyo Biblia inafundisha (K.v Mwanzo 1,1 Timotheo 6:13).

**Charles Darwin Aliona Uwezekano wa Dosari kwenye Nadharia Yake**

Inawezekuwa ya maana sana kukumbuka kwamba Charles Darwin,binadamu aliyepewa sifa kwa kinachoitwa maendeleo ya kisayansi

ya Nadharia ya mageuzi ( na kuwa kiufundi,mageuzi ni mfano wa kuigwa na siyo ya kisayansi),aliandika yafuatayo katika kitabu chake kiitwacho ‘’Asili ya aina’’-Origin of Species:

> Kama inaweza kuonyeshwa kwamba kiungo tata kimekuwepo ambacho hakingefanikiwa kuanzishwa na marekebisho mbalimbali mfululizo,basi nadharia yangu ingevunjika (Darwin C.The Origin of Species.In chapter 6,Difficulties on Theory.Cricket House Books LLC,2010 p.124).

Ingawa hakuamini kwamba hayo yaliyoonyeshwa yalimridhisha wakati aliandika yaliyo hapo juu,ukweli ni kwamba uhai wa seli ulikuwa na utata sana kuliko vile alivyotambua.Hivyo maandishi ya Charles Robert Darwin yana makubaliano kwamba alifahamu utata ziada ungepinga nadharia yake (Pengine inafaa ikumbukwe kwamba uvumbuzi wa DNA ingeonekana kustahili kama utata wa kutosha ambao hakutambua).Kwa hakika,wanasayansi wanajua kwamba asidi ya amino isiyo na mpangilio haiwezi kuja na DNA.Na kwa sababu hili halikujulikana wakati wa Darwin,sasa linajulikana.

Darwin mwenyewe anaonekana kukiri kwamba uhai haungeanza peke yake.Anaonekana,kwa kiwango fulani,kutegemea historia ya Biblia katika kitabu cha Mwanzo kama vile alivyoandika:

> Kuna fahari katika mtazamo wa uhai na mamlaka yake kadhaa,baada ya kutiwa pumzi hapo awali na Muumba ili uhai uwe katika aina tofauti au aina moja.(The origin of species By Charles Darwin,2nd and subsequent editions).

Hivyo inaonekana Darwin alitambua kwamba uhai hauwezi kuanza mwenyewe bila Muumba (Mungu).

Wanamageuzi wa kisasa wanapuuzia hali halisi ya kibiolojia.Kuna miayo shimo pana,yenye mwanya na la kutenganisha kati ya UHAI na MAUTI.Mwanya mkuu kati ya wanaoishi na wafu ni MPANA,WA KUPUUZIWA,USIOWEZA KUPIMWA na binadamu,ambao wanamageuzi wanaweza ‘’kudhani’’ na KUKISIA,wakipendekeza ‘’nadharia’’ isiyodhahiri,za kipepo yasiyo na ufasili kuhusu vile uhai hata ya aina ya chini sana ‘’ulianza.’’

Hitimisho lisiloepukika na ya kimantiki ni kwamba kuwepo kwa uhai unahitaji mpaji wa uhai!

**Mungu Ndiye MPAAJI MKUU WA UHAI!**

1.Je,Mungu anaonyesha kwamba ana uzima ndani yake? Yohana 5:26.Je,alimpa KARAMA ya UZIMA WA MILELE kwa Kristo aliyefufuka? Mstari huo.

2.Je,Biblia inatuambia kwamba Mungu anatoa uzima wa muda na wa milele? Warumi 6:23, 1 Timotheo 6:13a.

**MAELEZO:**Kumbuka! ‘’uzima’’ ni KARAMA INAYOLETWA NA MUNGU PEKEE!

3.Je,Mungu kwa fundisho kuu anasema kwamba aliumba binadamu kutoka kwenye mavumbi ya ardhi na KUMPA uzima wa muda,UHAI WA KIMWILI? Mwanzo 2:7

**MAELEZO:**Mwenyezi Mungu aliye na uzima ndani yake,yeye aliye na uhai,ambaye ni uzima,ambaye ALIKUWEKO kabla ya vitu vyote,ALIMPA binadamu,wanyama na miti yote,uzima wenye tabia ya mzunguko ambao unawezesha kuzaliana kulingana na sheria zilizowekwa!

**MUNGU PEKE YAKE NDIYE MPAJI WA UZIMA!**

**''Mageuzi'' ya AINA?**

Kinachoitwa ''Sayansi'' ya mageuzi inatoa nadharia kwamba kila AINA ya uhai,AINA ya ndege,hapa duniani-viumbe vya nchi,maji na hewa-ulitoka kwenye seli MOJA ulio na kifaa cha seli unganishi.Ulichipuka kuwa na uhai kwa GHAFLA katika lami ya bahari lenye joto-bila usaidizi wowote kutoka kwa mungu ye yote.

Hasa,ni jinsi gani basi,sayansi inafundisha kwamba aina tofauti ya uhai,AINA ya ndege,AINA ya wanyama,AINA ya samaki,nk-walitoka kwa SELI HII YA AWALI?

Hapa,kwa ufupi,ni fundisho la Nadharia ya Mageuzi;seli moja ya sehemu moja ya seli ilizidishwa,PEKE YAKE,kwa seli nyingine.Seli hizi baadaye ziligeuka kuwa minyoo ambao walizidi kuzaliana hadi bahari ikaongezeka na minyoo wengi!

HEBU FIKIRIA! ETI ''UMETOKA'' kwa minyoo! Ni MATUSI gani hayo kwa akili ya mwanadamu!

Lakini tukiendelea,minyoo hawa waliendelea na kuzaa.Wengine walienda kwenye ardhi,wakapata mapafu ya kupumua nje ya maji,na wakawa viumbe vinavyoitwa vyura.Wengine wao waliishi ardhini,na hivyo mashavu yao yakapotea.Basi wakawa wanyama wa ardhini.Vyura wakendelea kuishi ndani ya maji na kwenye ardhi,wakitumia mashafu na mapafu.Na aina halisi ya uhai ulibaki ndani ya maji,wakiwa na mashavu pekee yake.

Mageuzi yanafundisha kwamba aina ya uhai huu wa awali uliendelea polepole ama kupitia mabadiliko.Kupitia kwenye ''sheria ya asili iliyoimarishwa ya TOFAUTI YA JAMII YA WANYAMA,''kila uhai polepole ukachukua tabia mpya.Wakaendelea polepole hadi aina ya maisha ya utata ya kimwili na pia hadi ukakamavu wa akili-mpaka WAKABADILIKA kuwa AINA TOFAUTI ya wanyama.

Kwa aina hii ya utaratibu na ''ovyoovyo'',aina ya wanyama watambao,baadaye kwa aina ya wanyama watembeavyo kwa miguu (mamalia) (Wanyama walio na uti wa mgongo,ambao wa kike wananyonyesha vitoto vyao) waliendelea vile inavyodhaniwa.Mchakato huu wa maendeleo ya hatua na kubadilika kutoka kwenye aina tofauti hadi nyingine mpaka inafika kiwango cha AINA ya juu ilidhaniwa kwamba iliendelea kwa muda wa mamilioni ya miaka!

Kuchipuka kwenye aina tofauti ya uhai kulifanyika miongoni mwa aina nyingi ya uhai hadi kinachofanana na nyani leo hii akakuwepo.Baadaye sokwe anayefanana na mwanadamu (ama jamii inayofanana) kisha baadaye-WANADAMU!

Mabadiliko ya mwanadamu kutoka kwa mnyama wa chini anayefanana na sokwe inaaminiwa kuwa yalienda kwa UTARATIBU,ya kwamba haiwezekani kueleza hatua waliochukua kubadilika kutoka kwa sokwe ili wawe wanadamu! Basi,kulingana na ''nadharia'' hii,HAKUNA MWANADAMU WA KWANZA ANAYEITWA ADAMU,VILE BIBLIA INAVYODHIHIRISHA! Na bado kwa njia nyingine,wanamageuzi wengi wanakubali kwamba wanadamu wote wametoka kwa mama wa awali,ambaye,aliitwa ''Hawa.''

Wanadamu wa kwanza kulingana na nadharia ya mageuzi,walikuwa wa porini waliokosa akili.Lakini mawazo yakaendelea polepole kuimarika na tabia zikakomaa-kwa hivyo wanadamu INADHANIWA kwamba WAMEPATA KUIMARIKA HADI LEO.Kwa vile ''bila mpangilio'' haiwezi kueleza dhana hii,wanajaribu kudai kwamba ''kuponea

chupuchupu kwa wafaao'' ndiko kulisababisha hii.

Hii ndiyo Sayansi ''inadhania'' kuhusu mwanzo wa binadamu na ''aina'' tofauti ya viumbe ambavyo tunaona hivi leo.Lakini MUUMBAJI wa uhai wote ANADHIHIRISHA VILE ALIURATIBISHA NA KUFANYA ''AINA'' ILI WASIRUKE MIPAKA ILIYOWEKWA NA MUNGU WAO!

**Biblia Inadhihirisha MWANZO KAMILI ya ''AINA''**

1.Je,Mungu anadhihirisha kwamba aliumba vitu vyote vya aina tofauti vya viumbe viishivyo? Ufunuo 10:6.

2.Je, ''AINA'' ya viumbe hawa wangezaana kwa aina TOFAUTI ya familia yao? Ama wangezaa kulingana na AINA ZAO? Mwanzo 1:11,24.Basi soma Mwanzo 1 yote.

**MAELEZO:**Mungu anadhihirisha kwamba alifanya dunia na vilivyomo kama nyasi,matawi na miti kulingana na AINA YAO.Na pia viumbe hai kulingana na AINA YAO.

Mwanzo 1 inadhihirisha kuwa Mungu aliteuwa kwamba kila kiumbe hai alichokiumba WAKATI WA WIKI ya uumbaji angezidi KUZAA KULINGANA NA AINA YAKE! Kirahi ''kulingana na aina yake'' kimerudiwa sana! ''Aina'' tofauti haingezaa aina MPYA kama vile nadharia ya ''MAGEUZI'' inavyofundisha.

3.Je,Waebrania 4:3b inaeleza kwamba Mungu alikusudiwa kuendelea kuumba AINA MPYA katika vizazi vyote? Ama ALIMALIZA uumbaji wake katika wiki ya uumbaji?

**MAELEZO**: ''Kazi ilimalizika tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu.''HAKUNA AINA MPYA ya uhai ambao ungekuwepo baada ya uumbaji.Sokwe angezidi kuzaa sokwe-SIYO kubadilika kuwa binadamu!

Mungu anasema kwamba aliumba AINA tofauti ya uhai KWA GHAFLA.Kwenye wiki moja aliumba KILA KITU.Hakuteuwa kwamba AINA mpya ya viumbe hai vingejitokeza katika siku zetu!

''NADHARIA'' ya ''MAGEUZI'' ya aina INAPINGANA NA Ufunuo WA UKWELI WA Mungu! Mageuzi na Biblia pamoja haiwezi kuwa sawa-mmoja ni UWONGO.Kristo alipokuwa akiongea kuhusu SHETANI,alisema ''Yeye ni MWONGO,na BABA ya uwongo huo'' (Yohana 8:44).Kuna chanzo cha Mungu wa ulimwengu na Nadharia ya Mageuzi yanayopinga Biblia! Shetani aliutia msukumo na kuendelea KUDANGANYA ulimwengu kwa kuamini nadharia hiyo! Lakini wakati wa Shetani unatoweka kwa upesi mno.Yesu Kristo yu karibu KUCHUKUA NAFASI ya ''Baba'' ya uwongo wote!

**Ushahidi wa Kisayansi Unadhibitisha Aina kwenye Biblia**

Yeyote anaweza kutoa madai! Lakini unapofika wakati wa KUDHIBITISHA madai haya,twapata jambo jingine.Pengine tunayo thibitisho ama hatuna.

Wacha tutathmini ushahidi ili tuone UNAODAI UKWELI unaothibitika-Neno la Mungu ama Nadharia ya Mageuzi ya ulimwengu ambao umetiwa msukumo na Shetani.Mungu alimwambia Nuhu achukue viumbe hai wa kiume na wa kike wa dunia, ''KULINGANA NA AINA YAO,'' na kuwaweka ndani ya safina kubwa ambayo angejenga (Mwanzo 7:1-9).Lakini aliye na shaka atauliza, ''safina ingebebaje viumbe vingi ikiwa kuna AINA nyingi ya wanyama leo hii?''

Hilo ni swali zuri! Jawabu rahisi lapatikana! Katika Mwanzo 1:19-20,twapata kuwa Mungu aliwaleta wanyama wote wa msituni na ndege wote kwa Adamu ili awape MAJINA.Idadi ya ''aina'' ya Mwanzo wakati wa uumbaji walikuwa WACHACHE kiasi kwamba Adamu

aliweza kuwapa majina siku hiyo hiyo! Hii inaonyesha kwamba ''aina'' za awali ya Mwanzo walikuwa WACHACHE kwa idadi.

Basi wanasayansi wamejifunza kwamba AINA MPYA ya Mwanzo ya uhai ambao unaishi hewani,baharini ama kwenye ardhi unaweza kuzalishwa kiasili.Mnamo mwaka 1900 Hugo De Vries,alipojaribu na Primose,akapata kwamba kutoka kwa AINA ya primrose ulitokea AINA TOFAUTI ya PRIMOSE ambayo hajawahi kuona.Yalichipuka kwa GHAFLA ovyoovyo kwa hatua,kwa KURUKA.Wakaruka nje miongoni mwa watoto wao. ''Mchakato huu aliuita ,'' Mabadiliko.'' (''Man,Time and Fossils,''Ruth Moore,Chapter 8,p.130).

Hivyo basi ndiyo maana tuna ndege WA AINA,mbwa hata wanadamu leo hii!Hayo pia yanaeleza kwa nini Mungu aliamuru Nuhu Kuweka kila ''aina'' ya kiumbe hai ndani ya safina.Kwa sababu bado kulikuwa na ''aina'' ya mwanzo MCHACHE katika siku za Nuhu.Tangu wakati huo aina hizi wamezaa IDADI KUBWA YA AINA! Mageuzi hayakuwepo tangu mafuriko.Lakini tumekuwa na mabadiliko ndani ya aina-mwonekano MPYA WA AINA sawa na aina ya Mwanzo.Neno la Mungu linaambatana na Sayansi ya UKWELI ''Si Sayansi ya uwongo'' (1 Timotheo 6:20,KJV).

Wanasayansi WAMEJARIBU kuthibitisha nadharia yao ya mageuzi na , ''Uzazi wa Kuchagua'' na masomo katika ''mabadiliko.'' Lakini haya hayathibitishi mageuzi! Yanathibitisha,vile tulivyoona,kuwepo kwa SHERIA za hakika,ambazo haziwezi kubadilishwa zinazoongoza uzazi wa wanyama wote na uhai wa miti,na kwamba sheria hizo zinafanya kazi kwa mipaka michache ambayo haiwezi kuzidishwa au kuvunjwa!

Wakati tuna uwezo wa kupanda na kupalilia AINA TOFAUTI MPYA katika ''AINA'' kuu,bado ni ''AINA'' SAWA na SIYO aina mpya ya uhai!Kuna AINA nyingi TOFAUTI katika jamii fulani,na hata kama ni wachache,mbwa wadogo kama vile Chihuahua wa Meksiko,na mbwa wakubwa kama vile Mt.Benard ama Dane Mkuu,BADO NI MBWA! Siye paka ama farasi,ama hawaonyeshi dalili ya kubadilika kuwa JAMII NYINGINE! Wote ni ya AINA MOJA!

Mkulima wowote anayefanya kazi katika konde lake,aliyepanda ngano ama mmea mengine,anajua baadhi ya thibitisho la uzazi wa kuchagua.

Wanasayansi wanaofanya kazi na nguruwe wa aina au wanyama wengine katika maabara anaweza kupanga mfano kamili wa jinsi jeni na kromosomu zitakavyokabiliana katika kuzaliana kwa baadhi ya wanyama kwa mujibu wa rangi yao na sifa mbalimbali.

Wana uwezo wa kuwaambiana mapema hasa vile vitoto vyao vinafanana! Tena jambo hili haliithibitishi chochote isipokuwa inaonyesha kuwepo kwa mwenye hekima yote,Mungu aliye na nguvu zote ambaye alifanya sheria hizi,na ambaye pia anadumisha sheria hizo! Hakika kwamba Mungu aliamuru nchi izae viumbe hai ''baada ya aina yake'' na amekuwa akitekeleza na kuendeleza sheria tangu jadi,ni THIBITISHO kuu la kuwepo kwa Mungu na ukweli wa Neno lake Takatifu!

**Ardhi KAMILIFU-Kabla ya Adamu Ikawa UHARIBIFU**

Nini hasa ilitokea kwa nchi kabla Mungu kuumba binadamu wa kwanza? Mungu mwenyewe ANAJUA-kwa vile alikuwepo? Binadamu wanaweza ''kudhania'' ama ''kufikiria'' tu hasa kilichotokea.

Mungu sasa anaenda kukuambia kuhusu asili ya dunia yetu na baadaye ukiwa wake-kipindi cha muda wa mamilioni au mabilioni ya miaka kabla hajaumba wanadamu wa kwanza.Imefunuliwa yote katika Biblia yako!

1.Ni nini JAMBO LA KWANZA Mungu anaonyesha katika Biblia? Mwanzo 1:1.Je,Mungu hapo awali aliumba dunia ''Si TUPU''-SI KATIKA MCHAFUKO? Isaya 45:18,KJV.

**MAELEZO:**Nchi iliundwa vizuri na kwa njia kamilifu,na malaika wote wakapiga kelele (Ayubu 38:4-7).Ilikuwa KAMILI KWA UTARATIBU.Hakikuwepo na MCHAFUKO.Aliiumba (dunia) SIYO BURE.Neno la Kiebrania katika maandiko ya awali matakatifu,liliotafsiriwa kwa Kimombo hapa ni ''bure'' na Kiebrania ni ''TOHU'' linalomaanisha ''ukiwa'' ama ''machafuko'' (Strong's Exhaustive Concordance of the Bible).

Kwa hivyo dunia yetu hapo AWALI haikuumbwa ''bure''-siyo ''tohu''-sio ''UKIWA,'' ilikuwa sehemu KAMILIFU.

2.Kumbuka kwamba Mwanzo sura ya 1,ni wakati halisi katika mlolongo huu.Basi kumbuka kwamba katika Mwanzo 1:2 mtazamo mwingine wa dunia yetu.Je,bado ilikuwa mahali kamilifu?

**MAELEZO**: ''Dunia ilikuwa (ama ikawa) HAINA UMBO tena ilikuwa TUPU;giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji.'' Neno la Kihibrania la ''haina umbo'' ni ''TOHU''- neno ambalo pia limetumika katika Isaya 45:18.Kwa hivyo Mwanzo 1:2 inatueleza vile dunia kamili ya awali ILIBADILIKA kwenye hali ya ''kukosa umbo.''ILIBADILIKA KUWA ''tohu''-IKAWA UKIWA! Mabadiliko makubwa ya mambo hayo yalitukia! Na hayo yote yakatukia KABLA Adamu na Hawa na viumbe wa ulimwengu wao hawajaumbwa.Mungu ALISISITIZA ukamilifu wa uharibifu kwa kusema,kwa kuongeza, ''dunia ilikuwa TUPU.'' Neno la Kiebrania ya ''utupu'' linamaanisha ''UHARIBIFU USIOTOFAUTISHWA''! DUNIA YETU KWA SABABU NYINGINE ILIKUWA SEHEMU YA UHARIBIFU USIOTOFAUTISHWA! KWA NINI?

Mungu anatoa jibu.Kumbuka kwamba Mungu amewapa Shetani na mapepo yake utawala juu ya nchi yetu.Shetani ndiye ''mungu'' wa ulimwengu huu (2 Wakorintho 4:4).Lakini jina la Shetani halikuwa ''Shetani'' tangu mwanzo ambalo linamaanisha ''Mshitaki.'' Alikuwa akiitwa ''Lusifa,'' ambalo linamaanisha ''Mleta Mwanga.''

Lusifa alipewa cheo na kupandishwa kwa nafasi ya kerubi aliyetiwa mafuta ya Mungu (Ezekieli 28:14).Mungu alimweka katika dunia kamilifu kabla ya Adamu na kumfanya Lusifa kuwa Mtawala juu ya MALAIKA WOTE.

Lakini Lusifa hakuridhika na nafasi yake kubwa ya mamlaka.Alitamani NGUVU ZAIDI NA MAMLAKA.Alitamani kwa uchoyo,kuchukua nafasi ya Mwenyezi Mungu kama Mtawala Mkuu wa ulimwengu! (Isaya 28:12-14).Alisema, ''NITAPAA juu kupitia mawingu,nitajifanyia kama Yeye Aliye juu sana'' (Mstari wa 14).

Hivyo Lusifa na theluthi moja ya malaika wa Mungu wakawa wasaliti! (Ufunuo 12:3-4).Wakapanda mbinguni kwa kujaribu kung'oa Mungu kwenye kiti chake cha enzi na kuchukua utawala wa ulimwengu mzima! (Isaya 14:13)

Lakini Lusifa ALISHINDWA! Yeye na malaika wa kipepo wakafukuzwa na Mungu na majeshi ya malaika waaminifu na wakatifu.Wakatupwa juu ya nchi hii na KUFUNGIWA kwa anga yake (Isaya 14:12;Yuda 6) (Somo linalokuja linatarajiwa kukupa maelezo zaidi ya Lusifa kabla utawala wa Adamu duniani na baadaye uasi).

Shetani ALIMWASI Mungu.Alitenda dhambi dhidi ya Muumba Wake! Kuasi-yaani dhambi-huleta uharibifu kutoka kwa Mungu katika eneo ambalo dhambi imetokea.Ushahidi wa ukweli ni kufutiliwa mbali na Mungu kwa miji

ya dhambi ya Sodoma na Gomora,kwa sababu ya dhambi yao ‘’ilikuwa ya kutisha’’ (Mwanzo 18:20).Babeli ya kale walipata hatma sawia kwa ajili ya dhambi zake.

Sasa inakuwa wazi kwa mtazamo tunao wa dunia yetu,baada ya kuumbwa kamili vizuri,inaonyesha ‘’uharibifu wa kutofautishwa’’ kwa sababu ya dhambi ya Shetani,Mungu alifutilia mbali uso wa dunia yetu uliokuwa kabla ya Adamu akitumia janga lenye nguvu za asili.Uhai wa mimea yote na wanyama waliopo kwenye uso wa dunia kamilifu kabla ya Adamu walipatikana katika janga hili kubwa na kuangamia!

UUMBAJI KAMILI NA UHARIBIFU KAMILI ulitokea katika mistari miwili ya Mwanzo 1! Mungu ametuambia hivyo!

Ni nini tena kilitokea kwa dunia yetu wakati ilibaki ukiwa na ya giza? Mtu hawezi yeye mwenyewe kujua kwa uhakika.Lakini bado Mungu anatuonyesha kwa wakati unaofaa,Katika sura ya kwanza: ‘’Wakati huu Dunia ilikuwa haina umbo,tena ilikuwa tupu,giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji,naye Roho wa Mungu alikuwa ametanda juu ya maji.’’ (Mwanzo 1:2 sehemu ya mwisho na mstari wa 3).

Baada ya muda usiotambulika Mungu akaanza kuumba ulimwengu wa Adamu kwa kuweka eneo lake,katika Nyanja fulani,lililoharibika na kuliweka eneo hilo liweze kuwa maskani ya mwanamume na mwanamke wa kwanza.

Kumbuka kwamba Roho wa Mungu ‘’alikuwa ametanda juu ya MAJI’’ ulimwengu kabla ya Adamu uliharibiwa na kufunikwa na MAJI,sawia na dunia ya wakati wa Nuhu.Na kwa NGUVU ZA Roho Mtakatifu,Mungu alilitengeneza tena uso wa dunia,kama vile mistari hii ya Mwanzo 1 inaeleza.

**Muundo wa Miamba UNATHIBITISHA Ukweli wa Biblia**

Kwa kueleza mgawanyiko maalum ya dunia katika Uingereza uitwayo Mchanga mwekundu wa zamani,Hugh Miller anasema, ‘’Janga la kutisha lilisababisha uharibifu wa KIGHAFLA wa samaki kwenye eneo la karibu maili mia kutoka mpaka hadi mpaka----mabakio yanaonyesha alama ya kifo cha VURUGU.’’

Samaki wenye mafuta wakati mwingine hupatikana kwenye hali ya juu ya KUHIFADHI,inayoonyesha janga la KIGHAFLA lililotokea kabla ya Adamu! Mapezi magumu na midomo ilio wazi ya samaki wengi hawa wenye mafuta  inaonyesha TISHO LILILO DHAHIRI! Na papa ambao wana urefu wa futi tano waliuzika kiasi kwamba wananyooshwa kwa unene wa robo! Vile walivyozikwa inaonyesha wazi kwamba walikuwa wakijaribu kuogelea kwa hofu katika maji yaliyo na uzito na mashapo.

Kuhusu kina cha visukuku hivi,Lhwayd anasema, ‘’ visukuku vya bahari---ambavyo nimepata vimezikwa (ama vimefunikwa ndani ya jiwe imara  kwenye uso wa maporomoko ya bahari ya urefu wa pima 200.’’ UHARIBIFU wa maji ulibeba KINA KIKUBWA-KINA KIREFU KULIKO MAFURIKO YA NYAKATI ZA NUHU! Jinsi eneo la uso wa dunia umegawanywa haukujulikana.Lakini migodi mirefu na vipande vya milima inaonyesha kwamba dunia ilipangwa katika sehemu zingine kwa UREFU WA MAILI MBILI!

Kitendo cha mashapo yaliyojaa  maji ya uharibifu kabla ya Adamu kilitengeneza miundo mingi ya dunia vile tunavyoona hivi leo.Profesa Woodward wa chuo cha Cambridge alisema, ‘’ Dunia,kote ulimwenguni,unaonekana ukiwekwa wazi,umeundwa na migawanyiko inayoegemeana katika aina ya MASHAPO

mengi YALIYOANGUKA MFULULIZO NDANI YA MAJI.''

Mashapo haya mara nyingi yanageuka kuwa magumu kama mwamba.Safu zingine,zikiwa laini zinajikunja.Zingine baada ya kuwa ngumu ,zinapasuka.''Alama ya kiwimbi cha maji;; zinakuwa nyingi zaidi katika aina tofauti ya mawe.Na katika Migawanyiko hii ndiyo twapata mashapo ya makaa ya mawe,ambayo ni mabakio YALIYOGANDAMIZWA na janga kuu la uhai wa miti na wanyama walioishi kwa maisha mazuri kabla ya Adamu.

Kuna thibitisho kadhaa na ya uhakika ya mafuatano ya HARAKA ambayo migawanyiko kabla ya Adamu uliacha-ushahidi ambao wanamageuzi WANAKATAA KUAMINI.Miti mingi ya kitambo na mimea inapatikana,mara nyingi ikisimama WIMA,na kwa wakati mwingine katika msimamo mshazari-IKIPELEKA MIZIZI KUPITIA MIPANGILIO YA MAWE!

Mimea kama mikiafarasi,mikurupuko na mimea mingine laini sana inayoweza kuvunjika kwa urahisi.Na bado mimea hii inapatikana mahali PAGUMU PENYE MCHANGA,ikiwa haijavunjika na imeshikana! Makusanyiko ama utuaji wa mashapo yanayobebwa na maji YALIKUWA KWA UPESI,yalizuia kuoza kwa sehemu ya nje ya mimea hii! Mipangilio hii ilitengenezwa kwa siku-siyo miaka elfu ama mamilioni ya miaka!

Uharibifu wa uhai wa bahari na ardhi nyakati za uasi wa Lusifa inathibitishwa na migawanyo ya dunia.Wanajiolojia wanaita migawanyo hiyo inayobeba uhai wa bahari, ''Paloziki,'' na wa mimea, '' Mesoziki.''Migawanyo yote inayounda aina mbili ya uhai uliwekwa chini kwa ghafla.Mara nyingi ni NENE na MGUMU kuliko mashapo ya gharika ya Nuhu.

Ni jambo la kuvutia sana kutambua kwamba ulimwengu kabla ya Adamu umeitwa kwa jina linalofaa yaani, '' Nyakati za wataambazi/reptilia. ''Wataambazi wakubwa-wengine ambao walikuwa wakizurura ardhini na pia wakiruka hewani, wakati wengine walikuwa wakitumia samaki ndani ya bahari! Wadudu wakubwa walikuwa wamejaa hewani.Miti ya kangaga mikubwa,majani ya mabwawa na mimea mingine ilifunika uso wa dunia,na kufanya misitu tunayojua leo hii.

Lakini katika kitabu cha Mwanzo sura ya 1,tunao maelezo ya uumbaji wa ajabu Mungu aliufanya kulingana na mahitaji ya wanadamu.Wanyama wanaozaa wa kila aina,pamoja na wanaofugwa waliumbwa (mistari ya 24-25).Hata nafaka za makonde,matunda na mboga yaliumbwa kwa ajili ya binadamu (mistari 11-12,29).

Wanasayansi wanakubali kwamba wameduwazwa na muonekano wa KIGHAFLA wa wanyama hawa katika rekodi ya zamani na kupotea KIGHAFLA ya aina ya uhai ambao ulikuwa katika ulimwengu wa Lusifa.Sikia vile mmoja anavyofikiri:

> G.G.Simpson alisema kwamba vituko vya ajabu na kwa njia nyingi ''tukio la ajabu sana katika historia ya uhai wa dunia ni mabadiliko kutoka kipindi cha mesoziki ya wataambazi/reptilia hadi kipindi cha wanyama wazaao/mamalia,Inaonekana kwamba pazia ilitolewa GHAFLA kwenye kituo ambacho majukumu muhimu yalichukuliwa na wataambazi/reptilia,haswa dinosau,katika idadi kubwa na aina tatanishi,na kuchipuka tena MARA MOJA kufunua mazingira sawia lakini umbo ambalo dinosau hawangepatikana nalo kabisa.Wataambazi kawaida wanaigiza sehemu ndogondogo lakini sehemu nyeti zinatumika na mamalia/wanyama wazaao na

kunyonyesha...'' (Historic Geology,Carl O.Dunbar,Page 426).

Baadhi ya AINA YA WAWAKILISHI wa ulimwengu wa Lusifa wameishi,lakini ''kipindi kikubwa cha wataambazi kilipitwa na wakati! Ulimwengu sasa ni ya wanadamu kuzaana na kutawala (Mwanzo 1:26).Lakini binadamu alifanya ufisadi kwenye njia zake na KUTENDA DHAMBI zaidi (Mwanzo 6:5,12-13).Mnamo takriban miaka 1650 baada ya Adamu na Hawa kuumbwa,Mungu alitumia gharika kuharibu wanyama wote wanaopumua,ila Nuhu na wote waliokuwa ndani ya safina.

**Gharika ya Nuhu ILITOKEA**!

Wanamageuzi WANAKANA rekodi ya Biblia ya gharika iliofanyika wakati wa Nuhu.Lakini kuna thibitisho kwamba Gharika ilitokea.

1.Je,Mungu anadhihirisha,kupitia kwa Neno lake Takatifu-yaani Biblia kwamba kulikuwako na gharika katika nyakati za Nuhu? Soma Mwanzo sura 6,7 na 8.

2.Je,Mungu anasema nini kuhusu WAFANYA DHIHAKA ambao wana shaka kuhusu kuwepo kwake na nguvu zake? 2 Petro 3:3-6

**MAELEZO:**Mungu anasema hapa kwamba wanaodhihaki katika nyakati zetu watazidi kuwa wajinga-bila kujali kuona ushahidi wa THIBITISHO la kuwepo kwa Mungu,uumbaji wake wa ulimwengu na UKWELI kwamba Gharika ya Nuhu ilitokea!

Ni nini basi,THIBITISHO la gharika ya Nuhu? Maji yaliyofunika ulimwengu wakati wa Nuhu yaliacha ALAMA ZINAZOONEKANA kwenye nchi.Nguvu za mmomonyoko ya maji ya gharika yaliyopungua na maji yenye nguvu na mashapo yalizika mabilioni ya wanyama na miti! Mabakio yao yamepatikana ULIMWENGUNI KOTE-ushuhuda usioongea wa uharibifu ulioletwa duniani kwa sababu ya dhambi ya wanadamu.

Malezi moja ya miamba katika Bara Afrika,kwa mfano,yamekadiriwa kubeba mifupa milioni elfu mia nane (800,000,000,000) ya wanyama wenye uti wa mgongo! (Journal of Paleontology,May 1959,p.496.)

Wanajiolojia wanafanya utafiti na kuchambua ushahidi huu kila siku,hata hivyo maana ilio wazi ya matokeo ya utafiti yanapuuzwa! Badala yake,Nadharia ya Mageuzi isiyo na msingi inafanya mtu kuamini kuwa viumbe hawa walizikwa pole pole baada ya mamilioni ya miaka! Bado mwanajiolojia ye yote lazima anakubali kwamba mnyama lazima azikwe haraka na mashapo,ama kwa mbinu nyingine,ama MIFUPA yake haitakuwa kisukuku.Mamilioni ya wanyama wanaoitwa baisani waliuawa kwenye nchi tambarare mkuu kule Marekani mnamo mwisho wa karne ya 20,hata hivyo HATA MMOJA hakugeuka kuwa kisukuku.Mfano ulio dhahiri gharika kubwa ilizika mabilioni ya viumbe ambao wanasayansi walipata chini ya miamba!

Uzuri ni kwamba mashapo yote ya gharika ya wakati wa Nuhu yalikuwa MEMBAMBA na yalitawanyika kwenye uso wa dunia.Wanajiolojia wanayaita baadhi ya mashapo haya ''senoziki.''

**''Sayansi'' INATAFSIRI VIBAYA Ushahidi**

Katika Mwanzo sura ya 7 na 8,Mungu anaonyesha kwamba Gharika ya wakati wa Nuhu iliendelea POLE POLE.Ilianza na siku 40 ya mvua.Maji ya gharika yalifika kileleni mnamo mwezi wa saba wa mwaka na yakachukua muda huo kupungua.

Lakini mikondo yake ya maji HAIKUWA NA VURUGU KILA MAHALI,kwa sababuMungu alilinda safina (Mwanzo 8:1),na upepo ukandoa mafuriko.Kwa hivyo,mashapo kutoka kwa Gharika ya Nuhu hayakuwa marefu kama yale yalioachwa kwa ulimwengu kabla ya Adamu.

Kuna ufahamu wa kawaida leo hii kwamba visukuku vingi vinachimbwa kutoka kwenye VINA VIREFU! Vingine vinawakilisha uhai wa bahari.Vingine ni hayawani wakubwa ambao hatuna rekodi yao.

Ni uumbaji TOFAUTI-UUMBAJI MWINGINE ULIOZIKWA KWENYE KINA KIREFU-AMBAO WALIKUWA SEHEMU YA UUMBAJI WA ADAMU uliozikwa katika siku za Nuhu.Madhehebu mengine yanajumuisha UUMBAJI HUU ULIOZIKWA KWA KINA KIREFU na uumbaji wa nyakati za Adamu.

Uumbaji huu,uliozikwa kwenye kina kirefu unaonyesha nini?

Kwa nini janga kubwa lilileta madhara katika nchi yetu iliyokuwa kamili hapo awali kwa sababu ya DHAMBI YA LUSIFA,bila shaka!! UHARIBIFU KABLA YA ADAMU.

Mambo yanakuwa rahisi na wazi tukitathmini KWA MAKINI migawanyo ya dunia.Tunapata kwamba BIBLIA IMEBEBA UKWELI TANGU AWALI. SAYANSI PEKEE NDIYO IMEKUWA NA UZITO WA KUELEWA NA KUKUBALI UKWELI!

Mungu ametumia uumbaji wake wote KUTHIBITISHIA WANADAMU kuwa Biblia inamaanisha KWA HAKIKA inayosema.Kwanza Mungu anamwambia binadamu kwa wazi sana katika Mwanzo yaliyo ukweli.ALAFU anamwambia binadamu athibitishe Neno lake kupitia vitu vyote alivyoumba-uumbaji wake.

> 20 Kwa sababu mambo yake yasioonekana tangu kuumbwa ulimwengu YANAONEKANA na KUFAHAMIKA kwa kazi zake (uumbaji wa Mungu);yaani uwezo wake wa milele na uungu wake;hata wasiwe na udhuru.(Warumi 1:20).

Maelezo yako hapo,lakini wengi hawapendi kukubali hayo.

Wanamageuzi,bila shaka,wamekuja na mabishano tofauti wakijaribu kutetea msimamo wao.Lakini kupitia tathmini zaidi,mabishano yao hayana uchunguzi wa kisayansi wa kudumu.

Suala la Machi 1,2008 la Mwanasayansi Mpya linaeleza yafuatayo:

> ‘’Bado wazo linaendelea kwamba rekodi ya visukuku ina kiraka sana na haiwezi kuthibitisha mageuzi.Sababu moja ni ushawishi wa uumbaji.Kwanza kabisa kwa mbinu zao ni kupotosha ama kuupuzia uthibitisho wa mageuzi;uwongo uliopendwa ni ‘’hakuna mabadiliko ya visukuku/nishati.’’ Huu ni uwongo ulio wazi.

‘’Waumbaji hawana jawabu kwa uthibitisho usiopingika!’’

Bila shaka yaliyo juu hapo ni uwongo.

Historia ya ‘’thibitisho la wanamageuzi imekuwa ni ushahidi’’ uliotungwa,uwongo na kupuuzia sheria ya Sayansi.

Nikiongea juu ya thibitisho iliotungwa,nakumbuka nikitazama michoro ya viinitete vya wanadamu na wanyama wengine katika nakala ya Sayansi shuleni,na baadaye nikapata kujua kwamba michoro hio haikuwa sahihi,lakini ilibadilishwa ili viinitete hivyo vifanane ili waunge mkono ‘’mageuzi.’’

Naweza kumbuka nikitazama picha za nondo mweusi kwenye miti kule Uingereza ambao ilithibitisha kipengele cha mageuzi kisha baadaye nikagundua kwamba nondo hao hawaishi kwenye miti na walibandikwa kwenye miti kimakusudi ya kufanya picha ya kutoa thibitisho ya mageuzi.

Zaidi ya hayo,mafuvu ya vichwa vya awali yaitwayo ‘’kiungo kilichopotea’’ yaliyodai ‘’mageuzi’’ ya wanadamu yalipatikana kuwa ni

ulaghai hata kama wanasayansi wanaokubaliana na mageuzi walikubali uthibitisho huu kwa muda wa miongo mingi.

Je,ni nini kuhusu ''mabadiliko ya visukuku'' Mabishano ya Mwanasayansi Mpya? La muhimu ni kwamba inaonekana wanamageuzi wengi wanatumai kuwa WAKIDAI visukuku/nishati ni ''jamii inayobadilika,'' basi madai haya yanathibitisha kwamba kulikuwa na ''jamii inayobadilika'' nyingi (ambazo hawawezi kutoa ushahidi kamili kuhusu madai hayo) na kwamba mageuzi ni ya ukweli.

Lakini mageuzi kwa hakika hayajatoa ushahidi.Zaidi ya hayo,dhana ya jamii ''inayobadilika'' inakiuka moja ya kanuni ya mageuzi.Na dhana hiyo ni kuwa kiumbehai kinaendelea tu mahali kinaweza kuishi vizuri,ama kwa njia nyingine (kulingana na wanamageuzi) kuna kukua ovyo ovyo kwa hivyo wanaofaa ndio wanaishi,basi hakuna sababu halisi inayofanya jamii/spishi ''ibadilike.''

Anayeitwa ''kisukuku kinachobadilika anafaa awe mtambaazi/reptilia aliye na manyoya,na anathibitisha madai kuwa wataambazi waligeuka kuwa ndege.Jambo hili pia lilikuwa kwenye kitabu nilichokuwa nacho shuleni na kauli hii pia imethibitishwa kuwa ni uwongo.Tazama habari zifuatazo kuhusu kauli hiyo:

> Paris-wataalamu wa visukuku wamekanusha madai ya kisukuku ambacho kimekuwa ni uhakika uliothibitisha nadharia kwamba ndege walitoka kwa aina ya mnyama aitwaye dinosau.
>
> Mtazamo mfululizo wa sinosoroptariki,kisukuku kilichopatikana mwaka wa 1994 na mkulima katika mkoa wa Liaoning,Kaskazini Mashariki wa China,hazina ya awali ya kipindi ambapo miamba ya chaki iliumbika miaka milioni 130 iliyopita.....

Lakini utafiti mpya,uliochapishwa na kundi la wasomi wa Afrika Kusini linaloitwa Theagarten Lingham-Soliar katika chuo kikuu cha KwaZulu-unakana madai yaliyowekwa mbeleni ya manyoya miundo inayo matawi mawili,yanayoitwa kishore kinachopatikana kwa unyoya yaliyodaiwa awali kwamba yalikuwa manyoya,ni mabakio yasiyokuwa na madaha ya nyuzi za kolajeni ambazo zinaunganisha kichwa na mkia wa dinosau,vile wanavyosema.

Uthibitisho unatoka kwa sampuli iliyogunduliwa hivi karibuni ya sinosoptariki,pia inapatikana hapo,Rasilimali ya Yiksiani katika Liaoning,Ligham Soliar uliowekwa uchunguzi kwenye darubini iliyo na nguvu.

Ndege wa kwanza kujilikana ni akiopteriki,aliyeishi miaka milioni 150 iliyopita.Kinachokosekana ni uhusiano kati ya akiopteriki na jamii wengine ambao wangetuonyesha jinsi walibadilika.Lakini rekodi ya visukuku ni chache na haijakamilika na ndiyo maana mjadala umekuwa mkali sana.

Uthibitisho unaounga mkono manyoya duni ulikosa uchunguzi mkubwa,Ligham Soliar alisema.

> ''Hakuna hata uwakilishi hata kidogo wa muundo wa ngozi uliodaiwa kuwa manyoya ya awali,'' Ligham-Soliar anasema.

Inapatikana kwamba mageuzi ya manyoya yana maana sana katika

historia ya uhai, ''ugumu wa Sayansi unahitajika.''

Utafiti ulitokea Jumatano katika kumbukumbu la jamii ya kifalme B,makala ya Nasaba ya Kifalme,Chuo kisichopingika cha Uingereza cha Sayansi.
Na hata kama kulikuwa na manyoya,kwa vile wanasayansi pia wanakubali kwamba kiumbe huyu hakuruka,haileti maana kudai kwamba aligeuka kuwa kiumbe anayeweza kuruka.

Mageuzi yanajaribu mara nyingi kueleza uhai ulioanza bila muumbaji.Wazo ambalo sheria zingine za Sayansi zinapinga.

Ukweli unaohuzunisha ni kwamba mageuzi yamekubaliwa na wengi ambao hakika hawataki kuishi katika maisha ya kiungu,na hata hawatilii maanani maonyo ya unabii ulio katika Biblia.Hakika Biblia inaonyesha kwamba wanaoamini nadharia kama mageuzi wameruhusu mawazo yao kugeuka kutoka kwa ukweli na kuamini uwongo (Warumi 1:18-32).

**Mageuzi Dhidi ya Biblia**

Kumbuka kwamba dhana ya ulimwengu huu wa ''mageuzi'' ni NADHARIA tu au mfano wa maelezo.Neno ''Nadharia''linamaanisha ''TunaDHANI''! ''Nadharia'' siyo THIBITISHO LA UKWELI!

Basi,kwa vile wanataka kufanya kwamba ni ukweli,wanamageuzi watazidi kudai kwamba mageuzi ni mfano wa jinsi uhai uliendelea duniani.Lakini mfano huo bado unaegemea nadharia sawa.

''Nadharia'' ya mageuzi inadai kwamba dunia yetu ilikuwepo kwa mabadiliko yaliyoenda pole pole ya mata AMBAZO ZILIKUWEPO.Zaidi ya hayo,inafundisha kwamba mabadiliko haya yaliletwa kulingana na ''sheria asili zilizoimara,'' na nguvu zinazotoka NDANI ya kifaa chenyewe.

Mageuzi yanakanusha kwamba MUNGU alikuwa na mpango wa kubuni na kuumba dunia (ijapokuwa wanamageuzi wengine wanakubaliana na ''mageuzi ya Mungu'' ambayo inadai kwamba Mungu alianza na/ama akaongoza ''maendeleo ya mageuzi.'') Kwa vile Nadharia ya Mageuzi YANAKANA KABISA-Neno la Mungu ni wazi kwamba ni nadharia iliyotiwa msukumo na Shetani!

Biblia yako inasema kwamba MUNGU YUPO na kwamba ALIUMBA VITU VYOTE (Mwanzo 1:1)-kwamba Mungu alitumia mata kutoka NJE!
Tumeona kwamba Mungu alihakikisha uumbaji wake ungekuwa na THIBITISHO INAYOONEKANA-THIBITISHO LISILOGEUZWA-kwamba Biblia inasema UKWELI KAMILI!
Wacha tukumbuke ushahidi unaothibitisha kuwa Biblia ni YA KUTEGEMEWA,Neno lililotiwa msukumo na Mungu.

Basi twaona kwa NINI hakuna ulaini-HAMNA ''ulinganifu''-wa migawanyo ya nchi vile wanamageuzi WANAJARIBU kuthibitisha.Sasa twajua KWA NINI mabakio ya uhai wa wanyama na miti unapatikana kwenye migawanyo ya dunia yetu ambayo kitendo cha maji yaliyovurugika yangeleta-SIYO tendaji pole pole ya maji ambayo ingetokea ikiwa uso wa dunia ungeinuka POLEPOLE juu ya kiwango cha bahari na baadaye kuzama chini yake mara nyingi baada ya mamilioni ya miaka.

Vipindi vingine virefu vya jiolojia ya dunia dhahiri siyo vile wanavyodai wanajiolojia.Vipindi hivyo havingekuwa kabla mkondo MKALI wa maji na mzunguko wa maji wa KIGHAFLA ya janga lililotokea kabla ya Adamu lingezungusha aina tofauti ya udongo na vifusi.Mashapo haya yakatulia

haraka,kugandana na kuunda migawanyo tunayoiona leo hii.

HAKUNA siku mifupa ya wanadamu baada ya Adamu ilipatikana ndani ya migawanyo ya dunia pamoja na aina tofauti ya wataambazi ambao wanatambulika kuwepo ''nyakati kabla ya historia.'' Kwa nini? KWA SABABU HAWAKUWA WAMEUMBWA BADO!

Pamoja na idadi kubwa ya mifupa iliyotolewa kwenye ardhi ya tabaka tofauti,wanadamu hawajawahi KUTHIBITISHA hatua za ''mageuzi'' hata ya mnyama mmoja vile alivyobadilika kuwa mzuri na kufika umbo uliokomaa.HAKUNA MIFUPA KAMA HIYO ILIYOKUWEPO kwa sababu Mungu aliumba vitu vyote KIGHAFLA na ''MIANYA ya mageuzi'' inachipuka wakati jaribio kama hilo limefanywa.Uundaji mpya wa kawaida wa mifupa ya ''kimageuzi,'' mara nyingi na kwa hakika ni mkusanyiko wa mifupa TOFAUTI ya ''AINA'' SAWA ambayo ilizikwa kwa WAKATI MMOJA-siyo vipindi tofauti!

Uthibitisho wote unaonyesha kwamba BIBLIA INASIMAMA KAMA THIBITISHO LISILOPINGIKA NA HOJA ZAKE ZOTE.UUMBAJI WA MUNGU UNAMTHIBITISHIA!

**USIPUMBAZWE**

Mizaha kuhusu ''mageuzi'' kutoka kwa nyani hadi sokwe imenenwa kwa muda wa karne moja.Na wakati mwingine utaona katuni kuhusu binadamu anayeitwa ''wahenga''.Hii ni kwa sababu  ulimwengu umemeza NADHARIA ya mageuzi usiothibitika kama UKWELI.

Kutoka wakati mmoja hadi mwingine ''Wanasayansi'' wamedai uvumbuzi maarufu ambao mafundisho ya mageuzi YANADHANIWA kusafirishwa kutoka kwenye ulimwengu wa nadharia hadi ukweli.Miongi iliyopita,Wanasayansi walidai kupata sokwe ambao walikaribia kimo cha wanadamu wa kisasa.Kwa sababu sokwe hao wanakaribia kimo cha wanadamu na wanafanana kwa njia nyingine,wanasayansi wengine WAKACHUKUA kwamba walikuwa wahenga wa karibu sana wa binadamu.Wamekuwa wakibadilisha mtazamo huo,na pia mitazamo mengine ambao walifikiri ''itathibitisha'' mageuzi

Wakati watafiti walipata SOKWE wakubwa/NYANI,walipata pia kangaga WAKUBWA,kaa WAKUBWA,chui WAKUBWA na ndovu WAKUBWA! Ni ya kimantiki kwamba SOKWE wakubwa wangepatikana pia! Lakini bado ni sokwe sio  ''wanadamu.'' Kwa hivyo SOKWE WAKUBWA HAWATHIBITISHI chochote kuhusu yanayodhaniwa kama ''mageuzi'' kutoka kwa tumbili na sokwe!

Mara nyingi kwa njia moja au nyingine,dhana ya mageuzi inachochewa na vyombo vya habari.Na KUNA SABABU! Mageuzi inafanya kuamini Mungu na Biblia kutowezekana!

Mageuzi INAKANA umuhimu wa Muumbaji ambaye ni Mwenyezi Mungu.Inajaribu ''kufunga milango'' ya Yule aliyesema kwamba ni MUUMBA WA VITU VYOTE.Na inadokeza kuwa MUNGU HAJAWAHI KUWEPO.Na inafanya Biblia IONEKANE kama uwongo!

Mageuzi pia INAKANA umuhimu wa MKOMBOZI,kwa sababu bila Mungu basi hakuna Amri za Kiroho ZITAKAZOVUNJWA! HAKUNA ye yote atakayehitajika KUTII.Na mageuzi,kwa hivyo inakuongoza kuamini kwamba mauti ya mwili  ni ''mwisho wa njia'' yako!

Lakini Biblia inafundisha kwambaAdamu aliumbwa kamili kimwili hapo mwanzo.Aliumbwa KIGHAFLA.Inaonyesha kwamba yeye na Hawa waliasi Muumba wao-wakatenda dhambi-kwa hivyo wanahitaji Mkombozi atakayeondoa dhambi zao.Inafundisha pia kwamba wanadamu wanaweza kuupokea uzima wa milele kama KARAMA ya bure kutoka kwa Mungu kwa masharti kwamba wameungama dhambi

zao,kumkubali Yesu na KUMTII MUUMBA (Matendo 2:38)!

Leo hii,walimu na maprofesa katika nyanja zote za elimu wanaweka dhana ya MAGEUZI KATIKA MAWAZO YA VIJANA WETU.Inatambaa kama nyoka kwenye mizizi ya UKRISTO WA UKWELI! Hawataki wanafunzi kuzingatia kwamba kuna maelezo mengi ya kisayansi yanayokubalika kuwa yanaeleza jinsi uhai wa mwanadamu ulianza.


Uwongo wao unafanya kazi kwa mawazo ya mtoto ambaye hajafahamu sana,ukirudiwarudiwa mara nyingi hivi, '' Mungu hakumaanisha hivi aliposema KATIKA BIBLIA,'' 'Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi!'' Mawazo na ushawishi wa Shetani (Waefeso 2:2).Basi anatoa sababu hii, ''IKIWA maneno ya kwanza ya Biblia ni uwongo,basi BIBLIA MZIMA NI uwongo,'' ama, ''Biblia haiendi sambaba na yale Sayansi yanatueleza kuhusu mageuzi,basi Biblia LAZIMA ni ya uwongo.'' BAADAYE WENGI WANAGEUKA KUWA KAMA WAKAFIRI KABLA HAWAJAGUNDUA!

''Shetani aliyeudanganya ulimwengu wote'' (Ufunuo 12:9),alipanga hivyo! Kwa sababu ''Baba'' wa uwongo(Yohana 8:44) ndiye MTUNZI wa Nadharia ya Mageuzi!

Sasa unayo ukweli kutoka kwa Biblia na ''Sayansi'' ya UKWELI.Unayo THIBITISHO kamili kwamba uhakika uliopo kwa Biblia ni UKWELI.Uumbaji wa Mungu UNATHIBITISHA kwamba Biblia INATAKIKANA KUCHUKULIWA VILE ILIVYOANDIKWA!

Kozi ya Biblia itazidi kukuletea hakika hizi.Thibitisha na Biblia na Sayansi ya UKWELI na utajua kuwa UMEJUA BIBLIA INAMAANISHA YALIYOSEMWA!Swali ni je,wanamageuzi wana ufahamu sasa? Jibu:Wanakisia tu! Wanakisia vibaya kama vile wakanaji wa Neno la Mungu!

**Vidokezi Ishirini na Nane vya Maombi Yanayofaa:Sehemu ya 6**




*Kijitabu cha Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) kuhusu maombi*.

Na Bob Thiel.

*Hii ni sehemu ya sita ya sehemu nyingi mfululizo kuhusu maombi*.

Imesemekana kwamba ''Kanisa la Mungu linaendelea mbele kwa kupiga magoti.'' Msemo huu umekuwa ukitumika kama himizo kuwaambia Wakristo kwamba wanapaswa kuomba.Lakini kwa jinsi gani? Katika makala yaliyopita,maombi yalifafanuliwa na vidokezi ishirini na moja kujadiliwa.Katika makala haya,vidokezi vingine vitatu vimejadiliwa kuanzia kile kinachoitwa kidokezi ishirini na nne kimejadiliwa.

**Kidokezi 24:Mambo Magumu:Kumbuka Kufunga**

Mambo mengine yanaweza kuwa magumu.Unapaswa kufanya nini?

Kumbuka yafuatayo:

> 17 Mtu mmoja miongoni mwa ule umati wa watu akajibu, ''Mwalimu,nilimleta kwako mwanangu ambaye ana pepo mchafu anamfanya asiweze kuongea.18 Kila mara huyu pepo mchafu ampagaapo

mwanangu,humwangusha chini na kumfanya atokwe povu mdomoni na kusaga meno,kasha mwili wake hukauka.Niliwaomba wanafunzi wako wamtoe huyo pepo mchafu lakini hawakuweza.'' 19 Yesu akawaambia, ''Enyi kizazi kisicho na imani! Nitakuwa pamoja nanyi mpaka lini? Mleteni huyo mvulana kwangu.'' 20 Nao wakamleta yule mvulana.Yule pepo mchafu alipomwona Yesu,mara akamtia yule mvulana kifafa,akaanguka,akagaagaa chini huku akitokwa na povu kinywani.21 Yesu akamwuliza baba yake, ''Mwanao amekuwa akitokewa na hali hii tangu lini?Akamjibu, ''Tangu utoto wake.22 Mara kwa mara huyo pepo amekuwa akimwangusha kwenye moto au kwenye maji ili kumwangamiza.Lakini kama unaweza kufanya jambo lo lote,tafadhali tuhurumie utusaidie.'' 23 Yesu akamwambia, ''Kama ukiweza kuamini,yote yawezekana kwake yeye aaminiye.'' 24 Mara baba yake yule akapiga kelele akisema, ''Ninaamini.Nisaidie kutokuamini kwangu!'' 25 Yesu alipoona kwamba umati wa watu unakusanyika pamoja mbio,akamkemea yule pepo mchafu,akimwambia, ''Wewe pepo bubu na kiziwi,nakuamuru utoke wala usimwingie tena!'' 26 Yule pepo mchafu akiisha kupiga kelele,akamtia kifafa kwa nguvu akamtoka.Yule mvulana alikuwa kama maiti,hivyo watu wengi wakasema ''amekufa''.27 lakini Yesu akamshika mkono akamwinua,naye akasimama.28 Baada ya Yesu kuingia ndani ya nyumba,wanafunzi wake wakamwuliza wakiwa peke yao, ''Mbona sisi hatukuweza kumtoa huyo pepo mchafu?'' 29 Yesu akawajibu, ''Hali hii haiwezi kutoka isipokuwa kwa kuomba na kufunga.'' (Marko 9:17-29)

Kufunga ni kiungo cha maombi.Hali ngumu mara nyingi huhitaji kufunga pamoja na maombi.

Wakati mmoja kulikuwako na shida kwa kabila ya Benyamini,wana wa Israeli walichukua hatua ya kivita ambao Mungu alidhinisha (Waamuzi 20:18-20).Bado wana wa Israeli waliteseka mno (Waaamuzi 20:21).Na mateso haya yakafanyika mara ya pili (Waamuzi 20:25).Kwa hivyo,wana wa Isreali walichukua hatua pamoja na kufunga (Waamuzi 20:26-31),na wakashinda (Waamuzi 20:32-36).Wakati mwingine,hata kama maombi yanaenda sambamba na mapenzi ya Mungu,Mungu hajibu haraka,na kwa hivyo kufunga kunafaa.

Wakati Nehemia alisikia vile hali ilikuwa mbaya kule Yerusalemu,aliomba NA kufunga (Nehemia 1:4).Nehemia alikuwa tu mtu ambaye alimpelekea mfalme vinywaji (Nehemia 1:11).Na baada ya kuomba na kufunga,alisaidia na baadaye akawa Gavana wa Yuda (Nehemia 5:14;8:9).Watu walioishi Yerusalemu walikuwa na shida,na Mungu aliwapa msaada kupitia kwa mtu mmoja aliyeomba na kufunga.

Kumbuka pia:

> 6 ''Je! Saumu mliyoichagua,siyo ya namna hii? Kufunga vya uovu,kuzilegeza kamba za nira,kuwaacha nuru walioonewa,na kwamba mvunje kila nira? 7 Je! Siyo kuwagawia wenye njaa chakula,na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Umwonapo mtu aliye uchi umvike nguo wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe? 8 Ndipo utaita,na BWANA ataitika;utalia,naye atasema,Mimi

hapa.Kama ukiiondoa nira,isiwepo kati yako,wala kunyosha kidole,wala kunena maovu, 10 na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako,na kuishibisha nafsi iliyoyeswa,ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani;na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri.(Isaya 58:6-10)

Katika hali ngumu,usisahau kufunga.Biblia inapendekeza kufunga.

**Kidokezo 25:Omba Mungu na Kumshukuru**

Unapaswa kumshukuru Mungu katika maombi yako,na Mungu anataka ufanye hivyo:

> 8 Na wamshukuru BWANA,kwa fadhili zake,Na majabu yake kwa wanadamu.9 Maana hushibisha nafsi yangu shauku,Na nafsi yenye njaa huijaza mema. (Zaburi 107:8-9)

> 20 na kumshukuru Mungu Baba sikuzote kwa mambo yote,katika jina lake Bwana wetu Yesu Kristo;21 mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo. (Waefeso 5:20-21)

> 57 Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo.(1 Wakorintho 15:57)

> 17 Na kila mfanyalo,kwa neno au kwa tendo,fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu,mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye. (Wakolosai 3:17)

> 15 Basi kwa njia yake yeye,na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima,yaani,tunda la midomo iliungamayo jina lake. (Waebrania 13:15)

> 17 Nitakutolea dhabihu ya kushukuru;Na kulitangaza jina la BWANA (Zaburi 116:17)

> 6 Msijisumbue kwa neno lo lote;bali katika kila neno kwa kusali na kuomba.pamoja na kushukuru,haja zenu na zijulikane na Mungu; (Wafilipi 4:6)

Omba Mungu na kumshukuru!

Je,Mungu anataka umshukuru na kumsifu kwa sababu ubinafsi wake yuahitaji hivyo?

HAPANA.

Watu wengi hawaelewi mambo mengi kuhusu Mungu.Anataka ufanye hivi kwa sababu ni VYEMA kwako.

Kivipi?

Unapaswa kutambua kwamba dhambi zako hazijakudhuru peke yako lakini hata wengine.Licha ya haya,Mungu alituma mwanawe afe kwa ajili yako (Yohana 3:16) na yeye ndiye anakuhudumia.Ukweli ni kwamba unapaswa kushukuru.Sisi sote twafaa kumshukuru.

Zaidi ya hayo,shukuru kwa wito wako,Baraka zako za kiroho,uhai wako na Baraka za kimwili.Kitabu cha Zaburi kimejaa na vifaa vya kutumia kushukuru.Ungependa kusoma ili upate mawazo mengine ya kutoa shukrani.

**Vidokezi 26:Kabiliana na ''Dhambi ya Siri''**

Wakati mwingine una dhambi ambazo ziko njiani,pamoja na ya siri.Mungu hatakusikia ukikubali maovu:

> 18 Kama ningaliwaza maovu moyoni mwangu,Bwana asingesikia. (Zaburi 66:18)

> 1 Tazama,mkono wa BWANA haukupunguka,hata usiweze kuokoa

> wala sikio lake si zito,hata lisiweze kusikia;2 lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu,na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone,hata hataki kusikia. (Isaya 59:1-2)

Wengine wanafanya kazi mzuri ya kuzificha dhambi zao zisijulikane na wengine.Wengine hata wanaficha dhambi zao wasijue.Lakini anajua:

> 5 Ee Mungu,unajua upumbavu wangu,Wala hukufichwa yangu.(Zaburi 69:5)

> 7 Maana tumetoweshwa kwa hasira yako,Na kwa ghadhabu yako tumefadhaishwa 8 umeyaweka maovu yetu mbele zako,siri zetu zote zimepita katika hasira yako,Tumetoweshwa miaka yetu kama kite.( Zaburi 90:7-8)

Mungu atakuruhusu ukabiliane na majaribu ili akuondolee na kukusafisha dhambi zako:

> 2 Ndugu zangu,hesabuni ya kuwa ni furaha tupu,mkiangukia katika majaribu mbalimbali; 3 Mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi.4 Saburi na iwe na kazi kamilifu,mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa neno. (Yakobo 1:2-4)

Lazima tufanye bidii ili tuwe wakamilifu mbele ya Mungu,siyo mbele yetu.Yesu alifundisha:

> 48 Basi ninyi mtakuwa wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu. (Mathayo 5:48)

Hatuwezi kuzificha dhambi zetu mbele ya Mungu na inafaa tufanye bidii tusijifiche dhambi zetu.

Kumbuka vile Agano Jipya na Kale yanafundisha:

> 39 Mbona anung'unika mwanadamu aliye hai,Mtu akiadhibiwa kwa dhambi zake? 40 Na tuchunguze njia zetu na kuzijaribu,Na kumrudia BWANA tena 41 Na tumwinulie Mungu aliye mbinguni mioyo yetu na mikono. (Maombolezo 3:39-41)

> 27 Basi kila aulaye mkate huo,au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili,atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana.28 Lakini mtu ajihoji mwenyewe,na hivyo aule na kukinywea kikombe.29 Maana alaye na kunywa,hula na kunywa hukumu ya nafsi yake,kwa kutokuupambanua ule mwili.30 Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu,na watu kadha wa kadha wamelala.31 Lakini kama tungejipambanua nafsi zetu,tusingehukumiwa.32 Ili tuhukumiwapo,twarudiwa na Bwana,isije ikatupasa adhabu pamoja na dunia. (1 Wakorintho 11:27-32)

Lakini wanadamu huwa hawaamini jambo hilo.Tunafikiri shida zetu ni za kimwili na zinahitaji suluhisho la kimwili,wakati shida nyingi ni za kiroho na zinahitaji suluhisho la kiroho.

Hayo hayamaanishi kwamba tupuuzie za kimwili,lakini elewa pia kiroho:

> 7 Usiwe mwenye hekima machoni pako;Mche BWANA,ukajiepushe na uovu.8 Itakuwa afya mwilini pako,Na mafuta mifupani mwako.(Mithali 3:7-8)

> 2 Kwa nini kutumia fedha kwa kitu ambacho si chakula,na kuutabikia kitu kisichoshibisha? Sikilizeni,nisikilizeni

mimi na mle kilicho kizuri,nazo nafsi zenu zitafurahia utajiri wa unono.3 Tegeni sikio mje kwangu,nisikieni mimi,ili nafsi zenu zipate kuishi.Nitafanya Agano la milele nanyi,pendo la uaminifu nililomwahidi Daudi.(Isaya 55:2-3)

12 Na karibu na mto,juu ya ukingo wake,upande huu na upande huu,utamea kila mti wa chakula,ambao majani yake hayanyauka,wala matunda yake hayatatindika kamwe;utatoa matunda mapya kila mwezi,kwa sababu maji yake yanatoka mahali patakatifu,na matunda yake yatakuwa ni chakula;na majani yake yatakuwa ni dawa. (Ezekieli 47:12)

7 Bali hadithi za kizee,zisizokuwa za dini,uzikatae;nawe ujizoeze kupata utauwa.8 Kwa maana kujizoea kupata nguvu za mwili kwafaa kidogo,lakini utauwa hufaa kwa mambo yote;yaani,unayo ahadi ya uzima wa sasa,na ya ule utakaokuwepo baadaye. 9 Ni neno la kuaminiwa,tena lastahili kukubalika kabisa; 10 kwa maana twajitaabisha na kuhitahidi kwa kusudi hili,kwa sababu tunamtumaini Mungu aliye hai,aliye Mwokozi wa watu wote,hasa wa waaminio.11 Mambo hayo uyaagize na kuyafundisha. (1 Timotheo 4:7-11)

Jichunguze na ubadilike.Kumbuka Biblia inafundisha:

> 12 Kwa hiyo anayedhania kuwa amesimama na aangalie asianguke. (1 Wakorintho 10:12)

Sisi sote twahitaji imani zaidi na subira.Yesu hata aliuliza kama arudipo atapata imani duniani:


> 8 Nawaambia,atawapatia haki upesi;walakini,atakapokuja Mwana wa Adamu,je! Ataiona imani duniani? (Luka 18:8)

Yesu alitabiri kwamba kutakuwako na shida ya imani nyakati za mwisho.Sote tunahitaji imani zaidi,sote twahitaji kubadilika.

Mengi kuhusi maombi yanaweza kupatikana katika kijitabu chetu cha *Maombi:Biblia Inafundisha Nini?*

# Kuitekeleza Mathayo 24:14

# Pamoja na Mathayo 28:19-20



**Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG)**
**www.ccog.org**
**Taarifa za Unabii wa Biblia za kilasiku:**
**www.cogwriter.com**


CCOG.ASIA:Hii ni Tovuti ilengayo wasomaji kutoka Asia.Inazo makala katika lugha ya Kichina cha Mandarin pia na katika Kiingereza pamoja na lugha zingine za Kiasia.
CCOG.EU:Hii ni Tovuti kwa wale wa Ulaya.Inazo makala katika lugha nyingi za Ulaya.
CCOG.IN:Hii ni Tovuti inayolenga walio wa asili ya Kihindi.
CCOG.NZ:Hii ni Tovuti inayolenga walio wa asili ya New Zealand.
CCOGCanada.CA:Hii ni Tovuti ilengayo walio wa asili ya Canada.
CDLIDD.ES:Hii ni ya Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) katika lugha ya Kihispania.
PNHIND.PH:Hii ni Tovuti kwa ajili ya wale wa Ufilipino ama wenye asili yao.

YouTube

**Chaneli ya Habari za Unabii wa Biblia:**
**www.youtube.com/BibleNewsProphecy**

**Chaneli ya Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG):**
**www.youtube.com/continuingcog**

Mchungaji Mwandamizi wa Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) ni mgeni mwalikwa kwa mara kwenye redio, akitumia redio kuwafikia wasikilizaji wa maeneo mengi. Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) pia hutumia majarida pamoja na magazeti ya kielektroniki, vitabu na barua za kila juma kwa waumini wake katika kutekeleza Mathayo 24:14 pamoja na Mathayo 28:19-20.




Swahilie Edition